# 2 Wafalme

## *Hukumu ya Mwenyezi Mungu juu ya Ahazia*

1 Baada ya kifo cha Mfalme Ahabu, nchi ya
Moabu iliasi dhidi ya Israeli.
2 Basi Ahazia alikuwa ameanguka huko
Samaria kutoka baraza ya chumba chake cha juu,
akaumia. Hivyo akatuma wajumbe, akiwaambia,
“Nendeni mkaulize kwa Baal-Zebubu, mungu wa
Ekroni, mkaone kama nitapona kutokana na
kuumia huku.”
3 Lakini malaika wa Mwenyezi Mungu
akamwambia Ilya Mtishbi, “Panda uende
ukakutane na wajumbe wa mfalme wa Samaria,
uwaulize, ‘Je, ni kwa sababu hakuna Mungu
katika Israeli ndiyo maana mnaenda kumuuliza
Baal-Zebubu, mungu wa Ekroni?’
4 Kwa hiyo hili ndilo asemalo Mwenyezi
Mungu, ‘Hutaondoka kwenye kitanda unachokilalia. Hakika utakufa!’ ” Hivyo Ilya akaenda.
5 Wajumbe waliporudi kwa mfalme,
akawauliza, “Kwa nini mmerudi?”
6 Wakamjibu, “Mtu mmoja alikuja kukutana
nasi, naye akatuambia, ‘Rudini kwa mfalme
aliyewatuma na mkamwambie, “Hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu: Je, ni kwa sababu
hakuna Mungu katika Israeli ndiyo maana
unawatuma watu kwenda kuuliza kwa Baal-Zebubu, mungu wa Ekroni? Kwa hiyo hutaondoka kwenye kitanda unachokilalia. Hakika
utakufa!” ’ ”

7 Mfalme akawauliza, “Alikuwa mtu wa namna
gani ambaye mlikutana naye, akawaambia hili?”
8 Wakamjibu, “Alikuwa mtu aliyekuwa na
vazi la manyoya na mkanda wa ngozi kiunoni
mwake.”

Mfalme akasema, “Huyo alikuwa ni Ilya
Mtishbi.”
9 Ndipo mfalme akamtuma mkuu mmoja wa
kikosi pamoja na kikosi chake cha askari hamsini
kwa nabii Ilya. Yule mkuu wa kikosi akamwen-
dea Ilya, aliyekuwa ameketi juu ya kilima, na
kumwambia, “Mtu wa Mungu, mfalme anasema,
‘Shuka chini!’ ”
10 Ilya akamjibu yule mkuu wa kikosi, “Ikiwa
mimi ni mtu wa Mungu, moto na ushuke kutoka
mbinguni ukuteketeze wewe na watu wako ham-
sini!” Ndipo moto ukashuka kutoka mbinguni na
kuwateketeza yule mkuu wa kikosi pamoja na
watu wake.
11 Aliposikia hili, mfalme akatuma kwa Ilya
mkuu wa kikosi mwingine na askari wake ham-
sini. Yule mkuu wa kikosi akamwambia Ilya,
“Mtu wa Mungu, hili ndilo asemalo mfalme,
‘Shuka chini mara moja!’ ”
12 Ilya akajibu, “Ikiwa mimi ni mtu wa
Mungu, moto na ushuke kutoka mbinguni
ukuteketeze wewe na watu wako hamsini!”
Ndipo moto wa Mungu ukashuka kutoka mbin-
guni, ukamteketeza yeye na watu wake hamsini.
13 Hivyo mfalme akatuma mkuu wa kikosi wa
tatu na watu wake hamsini. Huyu mkuu wa
kikosi wa tatu akapanda na kupiga magoti mbele
ya Ilya, akiomba, “Mtu wa Mungu, tafadhali

niachie uhai wangu na uhai wa hawa watu hamsini, watumishi wako!
14 Tazama, moto umeshuka kutoka mbinguni
na kuwateketeza wale wakuu wa vikosi viwili vya kwanza pamoja na watu wao. Lakini sasa niachie uhai wangu!”

15 Malaika wa Mwenyezi Mungu akamwambia Ilya, “Shuka pamoja naye, usimwogope.” Hivyo Ilya akainuka na kushuka pamoja naye kwa mfalme.
16 Akamwambia mfalme, “Hili ndilo asemalo
Mwenyezi Mungu: Je, ni kwa sababu hakuna Mungu katika Israeli wa kumuuliza habari, ndiyo maana ukatuma wajumbe kuuliza Baal-Zebubu, mungu wa Ekroni? Kwa sababu umefanya hili, kamwe hutaondoka kwenye kitanda unachokilalia. Hakika utakufa!”
17 Hivyo akafa, sawasawa na lile neno la
Mwenyezi Mungu ambalo Ilya alikuwa amesema.

Kwa kuwa Ahazia hakuwa na mwana, Yoramu* akawa mfalme baada yake katika mwaka wa pili wa Yehoramu mwana wa Yehoshafati mfalme wa Yuda.
18 Kuhusu matukio mengine ya utawala wa
Ahazia na yale aliyoyafanya, je, hayakuandikwa katika kitabu cha kumbukumbu za wafalme wa Israeli?

# 2

### *Ilya achukuliwa mbinguni*

* **1:17** au *Yehoramu*

1 Mwenyezi Mungu alipokuwa karibu kum-
chukua Ilya mbinguni kwa upepo wa kisulisuli,
Ilya na Al-Yasa walikuwa njiani wakitoka Gilgali.
2 Ilya akamwambia Al-Yasa, “Kaa hapa.
Mwenyezi Mungu amenituma Betheli.”

Lakini Al-Yasa akasema, “Hakika kama Mwenyezi Mungu aishivyo na wewe uishivyo, sitakuacha.” Kwa hiyo wakaenda Betheli pamoja.

3 Wana wa manabii waliokuwa Betheli
wakamjia Al-Yasa na kumuuliza, “Je, unajua
kwamba Mwenyezi Mungu atakuondolea bwana
wako leo?”

Al-Yasa akawajibu, “Ndiyo, najua, lakini msizungumze kuhusu jambo hilo.”

4 Kisha Ilya akamwambia, “Baki hapa, Al-Yasa.
Mwenyezi Mungu amenituma Yeriko.”

Naye akajibu, “Kwa hakika kama Mwenyezi Mungu aishivyo na wewe uishivyo, sitakuacha.” Hivyo wakaenda Yeriko.

5 Wana wa manabii waliokuwa Yeriko
wakamwendea Al-Yasa na kumuuliza, “Je, unajua
kwamba Mwenyezi Mungu atakuondolea bwana
wako leo?”

Akawajibu, “Ndiyo, najua, lakini msizungumze juu ya jambo hilo.”

6 Kisha Ilya akamwambia, “Kaa hapa.
Mwenyezi Mungu amenituma kwenda Yordani.”

Naye akamjibu, “Kwa hakika kama Mwenyezi Mungu aishivyo na wewe uishivyo, sitakuacha.” Hivyo wote wawili wakaendelea pamoja.

7 Wana hamsini wa manabii wakaenda na
kusimama kwa mbali, kuelekea mahali Ilya na
Al-Yasa waliposimama kando ya Mto Yordani.

8 Ilya akatoa vazi lake, akalikunja na kupiga maji nalo. Maji yakagawanyika upande wa kuume na upande wa kushoto, nao wawili wakavuka pakavu.

9 Walipokwisha kuvuka, Ilya akamwambia Al-Yasa, “Niambie, nikufanyie nini kabla sijaondolewa kutoka kwako?”

Al-Yasa akajibu, “Naomba nirithi sehemu maradufu ya roho yako.”

10 Ilya akasema, “Umeomba jambo gumu. Lakini kama utaniona wakati ninapoondolewa kutoka kwako litakuwa lako. La sivyo, hutalipata.”

11 Walipokuwa wakitembea pamoja na kuzungumza, ghafula gari la farasi la moto na farasi wa moto vilitokea na kuwatenganisha wao wawili, naye Ilya akapanda mbinguni katika upepo wa kisulisuli.
12 Al-Yasa aliliona hili, naye akapaza sauti, “Baba yangu! Baba yangu! Magari ya vita ya Israeli na wapanda farasi wake!” Naye Al-Yasa hakumwona tena. Kisha akaishika nguo yake na kuirarua vipande viwili.

13 Akaliokota lile vazi lililoanguka kutoka kwa Ilya, kisha akarudi na kusimama ukingoni mwa Yordani.
14 Ndipo akalichukua lile vazi ambalo lilikuwa limeanguka kutoka kwa Ilya, naye akayapiga yale maji nalo. Akauliza, “Yuko wapi sasa Mwenyezi Mungu, Mungu wa Ilya?” Al-Yasa alipoyapiga maji, yakagawanyika kulia na kushoto, naye akavuka.

15 Wale wana wa manabii kutoka Yeriko
waliokuwa wakitazama wakasema, “Roho ya Ilya
inamkalia Al-Yasa.” Nao wakaenda kumlaki na
kusujudu hadi chini mbele yake.
16 Wakasema, “Tazama, sisi watumishi wako
tunao watu hamsini wenye uwezo. Waruhusu
waende kumtafuta bwana wako. Labda Roho
wa Mwenyezi Mungu amemtwaa na kumweka
katika mlima fulani au bonde fulani.”

Al-Yasa akajibu, “Hapana, msiwatume.”

17 Lakini wakasisitiza, hata akaona aibu
kuwakatalia. Hivyo akasema, “Watumeni.” Nao
wakawatuma watu hamsini, wakamtafuta kwa
siku tatu, lakini hawakumpata.
18 Walipomrudia Al-Yasa, aliyekuwa akingo-
jea huko Yeriko, akawaambia, “Je, sikuwaambia
msiende?”

### *Kuponywa kwa maji*

19 Watu wa mji wakamwambia Al-Yasa,
“Tazama, bwana wetu, mahali mji huu
ulipojengwa ni pazuri, kama bwana wangu
anavyoona, lakini maji yake ni mabaya, na nchi
haina mazao.”
20 Akasema, “Nileteeni bakuli mpya, mweke
chumvi ndani yake.” Kwa hiyo wakamletea.
21 Kisha akaenda kwenye chemchemi na
kuitupa ile chumvi ndani yake, akisema, “Hili
ndilo asemalo Mwenyezi Mungu: ‘Nimeyaponya
maji haya. Kamwe hayatasababisha mauti tena
wala kutozaa.’ ”
22 Nayo yale maji yakaponywa hadi leo, sawa-
sawa na neno la Al-Yasa alilokuwa amesema.

### *Al-Yasa afanyiwa mzaha*

23 Kutoka huko Al-Yasa akakwea kwenda
Betheli. Ikawa alipokuwa akitembea barabarani,
baadhi ya vijana wakatoka mjini na kumfanyia
mzaha. Wakasema, “Paa, wewe mwenye upara!
Paa, wewe mwenye upara!”
24 Akageuka, akawatazama na kuwalaani kwa
Jina la Mwenyezi Mungu. Kisha dubu jike
wawili wakatokea mwituni na kuwararua vijana
arobaini na wawili miongoni mwao.
25 Naye akaondoka huko, akaenda Mlima
Karmeli, na kutoka huko akarudi Samaria.

# 3

*Moabu wanaasi*

1 Yehoramu* mwana wa Ahabu akawa mfalme
wa Israeli katika Samaria mwaka wa kumi na
nane wa utawala wa Yehoshafati mfalme wa
Yuda, naye akatawala kwa miaka kumi na mbili.
2 Akafanya maovu machoni pa Mwenyezi
Mungu, lakini sio kama baba yake na mama
yake walivyokuwa wamefanya. Akaondoa nguzo
ya ibada ya Baali ambayo baba yake alikuwa
ameitengeneza.
3 Hata hivyo akashikamana na dhambi za Yer-
oboamu mwana wa Nebati, ambazo alisababisha
Israeli kuzitenda, wala hakuziacha.
4 Basi Mesha mfalme wa Moabu alikuwa mfuga
kondoo; naye akatakiwa kumlipa mfalme wa
Israeli ushuru wa wana-kondoo elfu mia moja, na
sufu ya kondoo dume elfu mia moja.
5 Lakini baada ya Ahabu kufa, mfalme wa
Moabu aliasi dhidi ya mfalme wa Israeli.

---

* **3:1** au *Yoramu*

6 Kwa hiyo wakati ule Mfalme Yehoramu akaondoka kutoka Samaria na kukusanya Israeli yote tayari kwenda vitani.
7 Akapeleka pia ujumbe ufuatao kwa Yehoshafati mfalme wa Yuda: "Mfalme wa Moabu ameasi dhidi yangu. Je, utaenda pamoja nami kupigana dhidi ya Moabu?"

Akajibu, "Nitaenda pamoja nawe. Mimi ni kama wewe, watu wangu ni kama watu wako, farasi wangu ni kama farasi wako."

8 Akauliza, "Je, tutashambulia kupitia njia gani?"

Akajibu, "Kupitia Jangwa la Edomu."

9 Hivyo mfalme wa Israeli akaondoka akiwa pamoja na mfalme wa Yuda na mfalme wa Edomu. Baada ya kuzunguka kwa siku saba, jeshi likawa limeishiwa maji kwa matumizi yao na kwa ajili ya wanyama waliokuwa nao.

10 Mfalme wa Israeli akapaza sauti, akasema, "Nini! Je, Mwenyezi Mungu ametuita sisi wafalme watatu ili tu kututia mikononi mwa Moabu?"
11 Lakini Yehoshafati akauliza, "Je, hayuko nabii wa Mwenyezi Mungu hapa, ili tuweze kumuuliza Mwenyezi Mungu kupitia kwake?"

Afisa mmoja wa mfalme wa Israeli akajibu, "Al-Yasa mwana wa Shafati yuko hapa. Ndiye alikuwa akimimina maji juu ya mikono ya Ilya."

12 Yehoshafati akasema, "Neno la Mwenyezi Mungu liko pamoja naye." Kwa hiyo mfalme wa Israeli na Yehoshafati pamoja na mfalme wa Edomu wakamwendea.

13 Al-Yasa akamwambia mfalme wa Israeli,
“Nina uhusiano gani nawe? Nenda kwa manabii
wa baba yako na manabii wa mama yako.”

Mfalme wa Israeli akajibu, “La, sivyo, kwa
sababu ni Mwenyezi Mungu ametuita pamoja sisi
wafalme watatu ili atutie mikononi mwa Moabu.”
14 Al-Yasa akasema, “Hakika kama Mwenyezi
Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni
aishivyo, ninayemtumikia, kama si kwa heshima
niliyo nayo kwa Yehoshafati mfalme wa Yuda,
nisingekujali hata kidogo.
15 Lakini sasa, nileteeni mpiga kinubi.”

Mpiga kinubi alipokuwa akipiga, mkono wa
Mwenyezi Mungu ukaja juu ya Al-Yasa,
16 naye akasema, “Hivi ndivyo asemavyo
Mwenyezi Mungu, ‘Chimbeni bonde hili lijae
mahandaki.’
17 Kwa kuwa hivi ndivyo asemavyo Mwenyezi
Mungu: Hamtaona upepo wala mvua, lakini
bonde hili litajaa maji, nanyi pamoja na ng’ombe
wenu na wanyama wenu wengine mtakunywa.
18 Hili ni jambo rahisi machoni pa Mwenyezi
Mungu. Pia ataitia Moabu mikononi mwenu.
19 Mtaushinda kila mji wenye ngome na kila
mji mkubwa. Mtakata kila mti ulio mzuri, mtaz-
iba chemchemi zote, na kuharibu kila shamba
zuri kwa mawe.”
20 Kesho yake asubuhi, karibu na wakati wa
kutoa dhabihu ya asubuhi, tazama, maji yakawa
yanatiririka kutoka upande wa Edomu! Nayo
nchi ikajaa maji.
21 Basi Wamoabu wote walikuwa wamesikia
kuwa wale wafalme wamekuja kupigana dhidi

yao. Hivyo kila mtu, kijana na mzee, ambaye angeweza kushika silaha akaitwa na kuwekwa mpakani.

22 Walipoamka asubuhi na mapema, jua likawa linamulika juu ya maji. Wamoabu waliokuwa upande wa pili wakaona maji ni mekundu, kama damu.

23 Wamoabu wakasema, “Ile ni damu! Lazima hao wafalme wamepigana na kuchinjana wao kwa wao. Sasa Moabu, twendeni tukateke nyara!”

24 Lakini Wamoabu walipofika kwenye kambi ya Israeli, Waisraeli wakainuka na kuwapiga hata wakakimbia. Nao Waisraeli wakaivamia nchi na kuwachinja Wamoabu.

25 Wakaiharibu miji, kila mtu akatupa jiwe juu ya kila shamba zuri hadi likafunikwa. Wakaziba chemchemi zote na kukata kila mti mzuri. Kir-Haresethi peke yake ndio uliobaki na mawe yake yakiwa mahali pake. Lakini hata hivyo watu waliokuwa na makombeo wakauzunguka na kushambulia.

26 Mfalme wa Moabu alipoona kuwa vita vimekuwa vikali dhidi yake, akachukua watu mia saba wenye panga ili kuingia kwa mfalme wa Edomu, lakini wakashindwa.

27 Ndipo akamchukua mwanawe mzaliwa wake wa kwanza, ambaye angekuwa mfalme baada yake, akamtoa kama dhabihu ya kuteketezwa juu ya ukuta wa mji. Ghadhabu ikawa kubwa dhidi ya Israeli; wakajiondoa kwake na kurudi katika nchi yao wenyewe.

# 4

*Mafuta ya mjane*

1 Mke wa mmoja wa wana wa manabii
akamlilia Al-Yasa, akamwambia, “Mtumishi
wako, mume wangu, amekufa, nawe unajua
alikuwa anamcha Mwenyezi Mungu. Lakini sasa
yule anayemdai anakuja kuchukua wanangu
wawili kama watumwa wake.”
2 Al-Yasa akamjibu, “Nitawezaje kukusaidia?
Niambie, una nini ndani ya nyumba yako?”

Akasema, “Mtumishi wako hana kitu chochote kabisa, isipokuwa mafuta kidogo.”

3 Al-Yasa akasema, “Zunguka kwa majirani
zako wote ukaombe vyombo vitupu. Usiombe
vichache.
4 Kisha ingia ndani na ujifungie mlango, wewe
na wanao. Mimina mafuta kwenye vyombo
vyote, na kila kimoja kinapojaa, kiweke kando.”
5 Yule mjane akaondoka na kujifungia ndani,
yeye na wanawe. Wao wakamletea vyombo,
naye akaendelea kumimina mafuta.
6 Vyombo vyote vilipojaa, akamwambia
mwanawe, “Niletee chombo kingine.”

Lakini mwanawe akajibu, “Hakuna chombo kingine kilichobaki.” Basi mafuta yakakoma kutiririka.

7 Yule mwanamke akaenda akamwambia yule
mtu wa Mungu, naye mtu wa Mungu akasema,
“Nenda ukayauze hayo mafuta ulipe madeni
yako. Wewe na wanao mnaweza kuishi kwa kile
kinachosalia.”

*Mwana wa Mshunami afufuliwa*

8 Siku moja Al-Yasa akaenda Shunemu. Huko kulikuwa na mwanamke mmoja mwenye cheo, naye akamsisitiza Al-Yasa aje kula chakula. Kwa hiyo kila mara alipitia pale, akaingia humo ili ale.
9 Akamwambia mumewe, “Ninajua kwamba huyu mtu ambaye anakuja kwetu mara kwa mara ni mtu mtakatifu wa Mungu.
10 Tutengeneze chumba kidogo juu darini na tuweke ndani yake kitanda na meza, kiti na taa kwa ajili yake. Kisha anaweza kukaa humo kila mara akija kwetu.”

11 Siku moja Al-Yasa alipofika, akapanda chumbani kwake na kulala humo.
12 Akamwambia mtumishi wake Gehazi, “Mwite huyo Mshunami.” Hivyo akamwita, naye akaja akasimama mbele yake.
13 Al-Yasa akamwambia mtumishi wake, “Mwambie huyu mwanamke, ‘Umetaabika sana kwa ajili yetu. Sasa utendewe nini? Je, tunaweza kuzungumza na mfalme au jemadari wa jeshi kwa niaba yako?’ ”

Akajibu, “Mimi ninaishi kwangu miongoni mwa watu wangu.”

14 Al-Yasa akamuuliza mtumishi wake, “Je, ni nini kinachoweza kufanyika kwa ajili yake?”

Gehazi akasema, “Hakika, hana mwana, na mume wake ni mzee.”
15 Ndipo Al-Yasa akasema, “Mwite huyo mwanamke.” Kwa hiyo akamwita, naye akaja akasimama mlangoni.
16 Al-Yasa akamwambia, “Mwaka ujao, wakati kama huu utabeba mwana mikononi mwako.”

Yule mama akapinga, akasema, “La hasha, bwana wangu! Usimdanganye mtumishi wako, ee mtu wa Mungu!”

17 Lakini yule mwanamke akapata mimba,
na mwaka uliofuata wakati kama ule ule akamzaa mwana, kama vile Al-Yasa alivyokuwa amemwambia.

18 Mtoto akakua, naye siku moja akamwendea
baba yake, aliyekuwa pamoja na wavunaji.
19 Akamwambia baba yake, “Kichwa changu!
Kichwa changu!”

Baba yake akamwambia mtumishi, “Mchukue umpeleke kwa mama yake.”

20 Baada ya mtumishi kumbeba na kumpeleka
kwa mama yake, mtoto akaketi mapajani mwa mama yake hadi adhuhuri, kisha akafa.

21 Mama akampandisha na kumlaza juu ya
kitanda cha yule mtu wa Mungu, kisha akafunga mlango, akatoka nje.

22 Akamwita mume wake na kusema, “Tafad-
hali mtume mmoja miongoni mwa mtumishi pamoja na punda ili niweze kwenda kwa mtu wa Mungu haraka na kurudi.”

23 Mume wake akamuuliza, “Kwa nini uende
kwake leo? Leo si mwandamo wa mwezi, wala si Sabato.”

Mwanamke akasema, “Yote ni sawa.”

24 Akatandika punda na kumwambia mtumishi
wake, “Mwongoze huyo punda. Usinipunguzie mwendo hadi nikuambie.”
25 Kwa hiyo akaenda na kumfikia huyo mtu wa
Mungu katika Mlima Karmeli.

Alipomwona kwa mbali, huyo mtu wa Mungu
akamwambia mtumishi wake Gehazi, “Tazama,
yule Mshunami!
26 Kimbia ukamlaki, umuulize, ‘Je, wewe hu-
jambo? Mume wako hajambo? Mtoto wako ni
mzima?’ ”

Akasema, “Kila kitu ni sawasawa.”

27 Alipomfikia huyo mtu wa Mungu pale mli-
mani, akashika miguu yake. Gehazi akaja ili
amwondoe, lakini yule mtu wa Mungu akasema,
“Mwache! Yuko katika uchungu mkubwa, lakini
Mwenyezi Mungu amenificha jambo hili na haja-
niambia kwa nini.”
28 Yule mwanamke akasema, “Je, bwana
wangu, mimi nilikuomba mwana? Je,
sikukuambia, ‘Usiamshe matumaini yangu’?”

29 Al-Yasa akamwambia Gehazi, “Jikaze viuno,
chukua fimbo yangu mkononi mwako na ukim-
bie. Ikiwa utakutana na mtu yeyote, usimsalimie,
na mtu yeyote akikusalimu, usimjibu. Ilaze
fimbo yangu juu ya uso wa mtoto.”

30 Lakini mama mtoto akasema, “Hakika kama
Mwenyezi Mungu aishivyo na wewe uishivyo,
sitakuacha.” Kwa hiyo Al-Yasa akainuka, akafu-
atana naye.

31 Gehazi akatangulia mbele na kuilaza fimbo
juu ya uso wa mtoto, lakini hapakuwa na sauti
wala itikio. Hivyo Gehazi akarudi kukutana na
Al-Yasa, na kumwambia, “Mtoto hajaamka.”

32 Al-Yasa alipofika kwenye ile nyumba, mtoto
alikuwa amelala juu ya kitanda chake angali
amekufa.

33 Akaingia ndani, akajifungia yeye na yule
mtoto, akamwomba Mwenyezi Mungu.
34 Kisha akapanda kitandani, akalala juu ya
yule mtoto, mdomo wake juu ya mdomo wa
mtoto, macho yake juu ya macho ya mtoto,
mikono yake juu ya mikono ya mtoto. Naye
alipojinyoosha juu yake, mwili wa mtoto ukapata
joto.
35 Al-Yasa akajiondoa juu yake na kuanza
kutembeatembea ndani ya chumba, kisha
akarudi tena kitandani na kujinyoosha tena
juu ya mtoto mara nyingine. Mtoto akapiga
chafya mara saba, akafungua macho yake.
36 Al-Yasa akamwita Gehazi na kumwambia,
“Mwite huyo Mshunami.” Naye akafanya hivyo.
Yule Mshunami alipokuja, Al-Yasa akasema,
“Mchukue mwanao.”
37 Akaingia ndani, akaanguka miguuni pa Al-
Yasa na kusujudu hadi chini. Kisha akamchukua
mwanawe na kutoka nje.

### *Mauti ndani ya chungu*

38 Al-Yasa akarudi Gilgali, nako huko ku-
likuwa na njaa katika eneo lile. Wana wa
kundi la manabii walipokuwa wanakutana naye,
akamwambia mtumishi wake, “Teleka chungu
kikubwa jikoni uwapikie manabii.”
39 Mmoja wao akatoka kwenda mashambani
kuchuma mboga na akapata mtango-mwitu.
Akachuma matango na kujaza nguo yake aliy-
oikunja ili kubebea. Aliporudi, akayakatakata
na kuyatumbukiza ndani ya chungu, ingawa
hakuna aliyejua ni nini.

40 Mchuzi ukagawiwa watu, lakini walipoanza kula, wakalia, “Ee mtu wa Mungu, kuna mauti ndani ya chungu.” Nao hawakuweza kula.

41 Al-Yasa akasema, “Leteni unga.” Akauweka ndani ya chungu na kusema, “Wagawie watu ili wale.” Wala hapakuwa na kitu chochote chenye madhara ndani ya chungu.

### *Watu mia wanalishwa*

42 Akaja mtu kutoka Baal-Shalisha, akimletea mtu wa Mungu mikate ishirini ya shayiri iliyookwa kutoka kwa nafaka ya kwanza, pamoja na masuke ya nafaka mpya. Al-Yasa akasema, “Wape watu ili wale.”

43 Mtumishi wake akamuuliza, “Nitawezaje kuandaa hii mbele ya watu mia moja?”

Lakini Al-Yasa akajibu, “Wape watu ili wale. Kwa maana hivi ndivyo asemavyo Mwenyezi Mungu: ‘Watakula na kusaza.’ ”

44 Basi akaiandaa mbele yao ile mikate, wakala na baadhi yake wakasaza, sawasawa na neno la Mwenyezi Mungu.

# 5

### *Naamani aponywa ukoma*

1 Wakati huu, Naamani alikuwa jemadari wa jeshi la mfalme wa Aramu. Alikuwa mtu mkuu mbele ya bwana wake na aliyeheshimiwa sana, kwa sababu kupitia kwake, Mwenyezi Mungu

alikuwa amewapa Aramu ushindi. Alikuwa
askari hodari, lakini alikuwa na ukoma.[*]

2 Siku hizo vikosi kutoka Aramu vilikuwa
vimeenda na vikawa vimemteka msichana ku-
toka Israeli, naye akamtumikia mkewe Naamani.
3 Akamwambia bibi yake, “Kama bwana wangu
angemwona nabii aliye huko Samaria! Angem-
ponya ukoma wake.”

4 Naamani akaenda kwa bwana wake na
kumwambia alichosema yule msichana kutoka
Israeli.
5 Mfalme wa Aramu[†] akamjibu, “Hakika,
nenda. Nitatuma barua kwa mfalme wa Is-
raeli.” Kwa hiyo Naamani akaondoka, akiwa
amechukua talanta kumi[‡] za fedha, shekeli elfu
sita za dhahabu[§], na mavazi kumi.
6 Barua aliyopelekea mfalme wa Israeli il-
iandikwa hivi: “Pamoja na barua hii ninamtuma
mtumishi wangu, Naamani, kwako ili uweze
kumponya ukoma wake.”

7 Mara mfalme wa Israeli alipomaliza kuisoma
ile barua, akararua mavazi yake na kusema, “Je,
mimi ni Mungu? Je, mimi naweza kuua na ku-
fufua tena? Kwa nini huyu mtu anamtuma mtu
ili mimi nipate kumponya ukoma wake? Tazama
jinsi anavyotafuta kuanzisha ugomvi nami!”

8 Al-Yasa mtu wa Mungu aliposikia kwamba
mfalme wa Israeli alikuwa amerarua mavazi

---

[*] **5:1** *ukoma* ni neno lililotumika kueleza magonjwa mbalimbali ya ngozi ambayo si lazima yawe ni ukoma halisi [†] **5:5** yaani *Shamu* [‡] **5:5** Talanta 10 za fedha ni sawa na kilo 340. [§] **5:5** Shekeli 6,000 za dhahabu ni sawa na kilo 70.

yake, akamtumia ujumbe huu: “Kwa nini umer-
arua mavazi yako? Mwamuru mtu huyo aje
kwangu, naye atajua ya kuwa yuko nabii katika
Israeli.”
9 Kwa hiyo Naamani akaenda, akiwa na farasi
wake na magari yake ya vita, na kusimama
mlangoni mwa nyumba ya Al-Yasa.
10 Al-Yasa akamtuma mjumbe kumwambia,
“Nenda uoge katika Yordani mara saba, na nyama
ya mwili wako itapona, nawe utatakasika.”
11 Lakini Naamani akaondoka akiwa
amekasirika, akasema, “Hakika nilidhani
kwamba angetoka nje, asimame na kuliitia jina
la Mwenyezi Mungu, Mungu wake, na kupitisha
mkono wake juu ya mahali penye ugonjwa ili
aniponye ukoma wangu.
12 Je, Abana na Farpari, mito ya Dameski,
si bora kuliko mito yoyote ya Israeli? Je,
nisingeweza kuoga ndani ya hiyo mito na ku-
takasika?” Basi akageuka na kuondoka kwa
hasira kuu.
13 Watumishi wa Naamani wakamwendea na
kumwambia, “Baba yangu, kama huyo nabii
angekuambia kufanya jambo lililo kubwa, je,
hungelifanya? Je, si zaidi sana basi, anapokuam-
bia, ‘Oga na utakasike!’ ”
14 Hivyo akashuka na kujizamisha ndani ya
Yordani mara saba, kama vile huyo mtu wa
Mungu alivyokuwa amemwambia, nayo nyama
ya mwili wake ikapona na kutakasika kama ya
mwili wa mvulana mdogo.
15 Kisha Naamani na wahudumu wake wote
wakarudi kwa yule mtu wa Mungu. Akasi-

mama mbele yake na kusema, “Sasa najua kwamba hakuna Mungu katika ulimwengu wote isipokuwa katika Israeli. Tafadhali sasa upokee zawadi kutoka kwa mtumishi wako.”
16 Nabii akajibu, “Hakika kama Mwenyezi Mungu aishivyo, ninayemtumikia, sitapokea kitu hata kimoja.” Ingawa Naamani alimsihi sana, yeye alikataa.
17 Naamani akasema, “Ikiwa hutapokea, tafadhali mtumishi wako na apewe udongo kiasi cha mzigo wa kuweza kubebwa na punda wawili, kwa sababu mtumishi wako hatatoa tena sadaka ya kuteketezwa na dhabihu kwa mungu mwingine isipokuwa Mwenyezi Mungu.
18 Lakini Mwenyezi Mungu na amsamehe mtumishi wake kwa kitu hiki kimoja: Bwana wangu atakapoingia kwenye hekalu la Rimoni ili kusujudu, naye akiwa anauegemea mkono wangu, nami nikasujudu huko pia, wakati nitakaposujudu ndani ya hekalu la Rimoni, Mwenyezi Mungu na amsamehe mtumishi wako kwa ajili ya jambo hili.”
19 Al-Yasa akamwambia, “Nenda kwa amani.”
Baada ya Naamani kusafiri umbali fulani,
20 Gehazi, mtumishi wa Al-Yasa mtu wa Mungu, akajiambia mwenyewe, “Bwana wangu amemwachia kirahisi sana Naamani, huyu Mwaramu*, kwa kutokupokea kutoka kwake vile alivyovileta. Hakika kama Mwenyezi Mungu aishivyo, nitamkimbilia na kupata kitu kutoka kwake.”

* **5:20** au *Mshami*

21 Hivyo Gehazi akaharakisha kumfuatilia
Naamani. Naamani alipomwona akikimbia kumwelekea, akashuka chini kutoka gari lake la vita na kwenda kumlaki. Akauliza, “Je, mambo yote ni sawa?”

22 Gehazi akajibu, “Mambo yote ni sawa.
Bwana wangu amenituma nikuambie, ‘Vijana wawili kutoka kwa wana wa manabii wamenijia kutoka nchi ya vilima ya Efraimu. Tafadhali wape talanta ya fedha† na mavazi mawili.’ ”

23 Naamani akasema, “Hakika, chukua talanta
mbili za fedha.” Akamsihi Gehazi azipokee, kisha akafunga talanta mbili za fedha katika mifuko miwili pamoja na mavazi mawili. Akawapa watumishi wake wawili mizigo hiyo, nao wakaibeba wakitangulia mbele ya Gehazi.

24 Gehazi alipofika kwenye kilima,
akavichukua vile vitu kutoka kwa wale watumishi na kuvificha ndani ya nyumba. Akawaaga wale watu, nao wakaondoka.

25 Kisha akaingia ndani na kusimama mbele ya
Al-Yasa bwana wake.

Al-Yasa akamuuliza, “Gehazi, ulikuwa wapi?”

Gehazi akajibu, “Mtumishi wako hakuenda popote.”

26 Lakini Al-Yasa akamwambia, “Je, roho yangu
haikuwa pamoja nawe wakati yule mtu aliposhuka kutoka gari lake la vita ili kukulaki? Je, huu ni wakati wa kupokea fedha au kupokea nguo, mashamba ya mizeituni, mashamba ya mizabibu, makundi ya kondoo na

† **5:22** Talanta ni sawa na kilo 34.

mbuzi, makundi ya ng'ombe, au watumishi wa kiume na wa kike?
27 Ukoma wa Naamani utakushika wewe na wazao wako milele." Kisha Gehazi akaondoka mbele ya Al-Yasa, mwenye ukoma, mweupe kama theluji.

# 6

### *Shoka laelea*

1 Wana wa manabii wakamwambia Al-Yasa, "Tazama, mahali hapa tunapokutana nawe ni padogo sana kwetu.
2 Twendeni Yordani, ambapo kila mmoja wetu anaweza kupata nguzo moja, nasi tujenge huko mahali petu pa kuishi."

Naye akawaambia, "Nendeni."

3 Kisha mmoja wao akasema, "Je, tafadhali, huwezi kufuatana na watumishi wako?"

Al-Yasa akajibu, "Nitakuja."

4 Naye akaenda pamoja nao.

Basi wakaenda Yordani, nao wakaanza kukata miti.
5 Mmoja wao alipokuwa anakata mti, shoka lilitumbukia kwenye maji. Akalia, "Ee bwana wangu, shoka lilikuwa la kuazima!"
6 Mtu wa Mungu akauliza, "Je, liliangukia wapi?" Alipomwonesha mahali penyewe, Al-Yasa akakata kijiti na kukitupa mahali pale, nalo shoka likaelea.
7 Akasema, "Lichukue." Kisha yule mtu akanyoosha mkono wake, akalichukua.

### *Al-Yasa awanasa Waaramu waliopofushwa*

8 Wakati huo mfalme wa Aramu alikuwa akip-
igana vita na Israeli. Baada ya kukubaliana na
maafisa wake, akasema, “Nitapiga kambi yangu
mahali fulani na fulani.”

9 Mtu wa Mungu akatuma ujumbe kwa mfalme
wa Israeli: “Jihadhari usije ukapita mahali pale,
kwa sababu Waaramu wanashuka huko.”
10 Kwa hiyo mfalme wa Israeli akatuma neno la
tahadhari mahali pale alikokuwa ameelekezwa
na mtu wa Mungu. Mara kwa mara Al-Yasa
alimwonya mfalme kwamba watu wawe macho
kwenye maeneo kama hayo.

11 Hili lilimfadhaisha sana mfalme wa Aramu.
Akawaita maafisa wake, akawauliza, “Je, hamta-
niambia ni nani miongoni mwenu aliye upande
wa mfalme wa Israeli?”

12 Mmoja wa maafisa wake akasema, “Mfalme
bwana wangu, hakuna hata mmoja wetu. Lakini
Al-Yasa, yule nabii aliye Israeli, humwambia
mfalme wa Israeli hata yale maneno unay-
ozungumza katika chumba chako cha kulala.”

13 Mfalme akaagiza akisema, “Nendeni, mkata-
fute aliko, ili niweze kutuma watu kumkamata.”
Taarifa ikarudi kwamba, “Yuko Dothani.”
14 Ndipo akatuma farasi na magari ya vita
na jeshi lenye nguvu huko. Walienda usiku na
kuuzunguka mji.

15 Kesho yake asubuhi na mapema, mtumishi
wa mtu wa Mungu alipoamka na kutoka nje,
jeshi, pamoja na farasi na magari ya vita, likawa
limeuzunguka mji. Mtumishi wake akasema,
“Ole wetu, bwana wangu! Tutafanya nini?”

16 Nabii akajibu, “Usiogope. Wale walio pamoja
nasi ni wengi kuliko wale walio pamoja nao.”

17 Kisha Al-Yasa akaomba, “Ee Mwenyezi
Mungu, mfumbue macho huyu mtumishi ili ap-
ate kuona.” Ndipo Mwenyezi Mungu akayafum-
bua macho ya yule mtumishi, naye akatazama
na kuona vilima vimejaa farasi na magari ya vita
yaliyowaka moto yamemzunguka Al-Yasa pande
zote.
18 Adui waliposhuka kumwelekea, Al-Yasa
akamwomba Mwenyezi Mungu: “Wapige watu
hawa kwa upofu.” Basi Mungu akawapiga kwa
upofu, kama Al-Yasa alivyoomba.

19 Al-Yasa akawaambia, “Hii sio njia yenyewe,
na huu sio huo mji. Nifuateni mimi, nami
nitawapeleka kwa huyo mtu mnayemtafuta.”
Naye akawapeleka Samaria.

20 Baada ya kuingia mjini, Al-Yasa akasema,
“Mwenyezi Mungu, yafungue macho ya watu
hawa ili wapate kuona.” Ndipo Mwenyezi Mungu
akayafungua macho yao, na walipotazama,
kumbe hapo ndipo walipojikuta, ndani ya
Samaria.
21 Wakati mfalme wa Israeli aliwaona, aka-
muuliza Al-Yasa, “Je, baba yangu, niwaue?”

22 Naye akajibu, “Usiwaue. Je, utawaua watu
uliowateka kwa upanga wako mwenyewe na
upinde wako? Wape chakula na maji ili wapate
kula na kunywa, na kisha wamrudie bwana
wao.”
23 Basi akawaandalia karamu kubwa, na baada
ya kula na kunywa, akawaaga nao wakarudi

kwa bwana wao. Hivyo, vikosi kutoka Aramu vikakoma kuvamia nchi ya Israeli.

### *Njaa katika Samaria iliyozingirwa*

24 Baada ya kitambo kidogo, Ben-Hadadi mfalme wa Aramu akaandaa jeshi lake lote akapanda kwenda kuizingira Samaria.
25 Kukawa na njaa kuu katika mji. Samaria ilizingirwa kwa muda mrefu, kiasi kwamba kichwa cha punda kiliuzwa kwa shekeli themanini* za fedha, na robo ya kibaba† cha mavi ya njiwa kiliuzwa kwa shekeli tano‡ za fedha.
26 Mfalme wa Israeli alipokuwa anapita juu ya ukuta, mwanamke mmoja akamlilia, “Bwana wangu mfalme, nisaidie!”
27 Mfalme akajibu, “Ikiwa Mwenyezi Mungu hakusaidii, nitakutolea wapi msaada? Je, ni kwenye sakafu ya kupuria? Au ni kwenye shinikizo la kukamulia zabibu?”
28 Kisha akamuuliza, “Kwani kuna nini?”

Yule mwanamke akamjibu, “Huyu mwanamke aliniambia, ‘Mtoe mwanao ili tupate kumla leo, na kesho tutamla mwanangu.’
29 Basi tukampika mwanangu na kumla. Siku iliyofuata nikamwambia, ‘Mtoe mwanao ili tupate kumla.’ Lakini akawa amemficha.”
30 Mfalme aliposikia maneno ya yule mwanamke, akararua mavazi yake. Naye alipoendelea kutembea ukutani, watu

---

* **6:25** Shekeli 80 za fedha ni sawa na kilo moja. † **6:25** Robo ya kibaba ni sawa na lita 0.3. ‡ **6:25** Shekeli 5 ni sawa na gramu 55.

wakamtazama, na ndani ya mavazi yake alikuwa
amevaa gunia mwilini mwake.
31 Akasema, “Mungu na aniadhibu vikali zaidi
ikiwa kichwa cha Al-Yasa mwana wa Shafati
kitabaki juu ya mabega yake leo!”
32 Wakati huu, Al-Yasa alikuwa ameketi ndani
ya nyumba yake, akiwa pamoja na wazee.
Mfalme akatuma mjumbe kumtangulia, lakini
kabla hajafika, Al-Yasa akawaambia wale wazee,
“Hammwoni huyu muuaji jinsi anavyotuma mtu
kukata kichwa changu? Tazama, wakati mjumbe
huyo atakapofika, fungeni mlango na mzuieni
asiingie. Je, vishindo vya nyayo za bwana wake
haviko nyuma yake?”
33 Alipokuwa angali bado anazungumza nao,
mjumbe akamfikia. Naye mfalme akasema,
“Maafa haya yanatoka kwa Mwenyezi Mungu.
Kwa nini niendelee kumngoja Mwenyezi Mungu
zaidi?”

# 7

1 Al-Yasa akasema, “Sikiliza neno la Mwenyezi
Mungu. Hivi ndivyo asemavyo Mwenyezi
Mungu: Wakati kama huu kesho, kipimo kimoja*
cha unga mzuri kitauzwa kwa shekeli moja ya
fedha†, na vibaba viwili vya shayiri kwa shekeli
moja ya fedha katika lango la Samaria.”
2 Yule afisa ambaye mfalme alikuwa anauege-
mea mkono wake akamwambia yule mtu wa
Mungu, “Tazama, hata kama Mwenyezi Mungu

* **7:1** Kipimo kimoja cha unga ni sawa na kilo 3. † **7:1** Shekeli moja ni sawa na gramu 11.

atafungua madirisha ya mbinguni, je, jambo hili litawezekana?”

Al-Yasa akajibu, “Utaona kwa macho yako mwenyewe, lakini wewe hutakula chochote kati ya hivyo!”

### *Mwisho wa kuzingirwa*

3 Basi kulikuwa na watu wanne wenye ukoma
katika ingilio la lango la mji. Wakaambiana,
“Kwa nini tukae hapa hadi tufe?
4 Tukisema, ‘Tutaingia mjini,’ mjini kuna njaa,
nasi tutakufa humo. Tukikaa hapa, tutakufa.
Kwa hiyo twende kambi ya Waaramu, tujisalim-
ishe. Wakituacha hai, tutaishi; wakituua, basi na
tufe.”
5 Wakati wa mapambazuko, wakaondoka na
kwenda kwenye kambi ya Waaramu. Walipofika
mwanzo wa kambi, hapakuwa na mtu,
6 kwa kuwa Bwana alilifanya jeshi la Waaramu
lisikie sauti kama ya magari ya vita, farasi
na jeshi kubwa, kiasi kwamba waliambiana,
“Tazama, mfalme wa Israeli ameajiri mfalme wa
Wahiti na mfalme wa Wamisri kuja kutushambu-
lia sisi!”
7 Kwa hiyo wakaondoka na kukimbia wakati
wa giza la jioni na kuacha mahema yao, farasi
wao na punda wao. Wakakimbia kuokoa maisha
yao na kuacha kila kitu ndani ya kambi kama
kilivyokuwa.
8 Wale watu wenye ukoma walipofika mwan-
zoni mwa kambi, wakaingia kwenye mojawapo
ya mahema. Wakala na kunywa, na kuchukua
fedha, dhahabu na nguo, wakaenda kuvificha.
Wakarudi na kuingia katika hema lingine, na

kuchukua baadhi ya vitu kutoka ndani yake na kuvificha pia.

9 Kisha wakaambiana, “Hili tunalolifanya sio
jema. Hii ni siku ya habari njema, nasi tunakaa kimya. Tukisubiri hadi mapambazuko, maafa yatatupata. Twendeni mara moja tukatoe habari hizi katika jumba la mfalme.”

10 Hivyo wakaenda mjini na kuwaita wal-
inzi wa langoni, wakawaambia, “Tulienda katika kambi ya Waaramu lakini hapakuwa na mtu huko, hata sauti ya mtu yeyote, ila farasi na punda waliofungwa, na mahema yaliyoachwa kama yalivyokuwa.”

11 Walinzi wa langoni wakatangaza habari ile
kwa sauti kuu, na taarifa hii ikatolewa ndani ya jumba la mfalme.

12 Mfalme akaamka usiku na kuwaambia
maafisa wake, “Nitawaambia kile Waaramu walichotufanyia. Wanajua kwamba tuna njaa, hivyo wameacha kambi yao ili kujificha mashambani, wakifikiri, ‘Kwa hakika watatoka nje ya mji, nasi tutawakamata wakiwa hai na kuingia ndani ya mji.’ ”

13 Mmoja wa maafisa wake akajibu, “Waamuru
watu wachache wakawachukue farasi watano kati ya wale waliobaki katika mji. Hatima yao itakuwa kama ya Waisraeli wote walio hapa. Watakuwa tu kama Waisraeli hawa ambao wanangoja kifo. Hivyo tuwatumeni wajue kumetendeka nini.”

14 Ndipo wakachagua magari mawili ya vita
pamoja na farasi wake, naye mfalme akawatuma wafuatilie jeshi la Waaramu. Akawaamuru

waendeshaji akisema, “Nendeni mkaone ni nini
kilichotokea.”
15 Wakawafuatia hadi Yordani, nao wakakuta
barabara yote ikiwa imetapakaa mavazi na
vyombo Waaramu walivyokuwa wamevitupa
walipokuwa wakitoroka. Basi wale wajumbe
wakarudi na kutoa taarifa kwa mfalme.
16 Kisha watu wakatoka na kuteka nyara kambi
ya Waaramu. Kwa hiyo kipimo cha unga mzuri
kikauzwa kwa shekeli, na vipimo viwili vya
shayiri kwa shekeli, kama vile Mwenyezi Mungu
alivyokuwa amesema.

17 Basi mfalme alikuwa amemweka yule afisa
ambaye mfalme alikuwa anauegemea mkono
wake awe msimamizi wa lango. Nao watu
wakamkanyaga walipoingia langoni, naye akafa,
kama vile mtu wa Mungu alivyokuwa ametan-
gulia kusema wakati mfalme alipofika nyumbani
mwake.
18 Ikatokea kama vile mtu wa Mungu
alivyokuwa amemwambia mfalme: “Wakati
kama huu kesho, kipimo kimoja cha unga mzuri
kitauzwa kwa shekeli moja ya fedha, na vibaba
viwili vya shayiri kwa shekeli moja ya fedha
katika lango la Samaria.”

19 Yule afisa alikuwa amemwambia yule mtu
wa Mungu, “Tazama, hata kama Mwenyezi
Mungu atafungua madirisha ya mbinguni, je,
jambo hili litawezekana?” Naye yule mtu wa
Mungu alikuwa amemjibu, “Utaona kwa macho
yako mwenyewe, lakini wewe hutakula chochote
kati ya hivyo!”

20 Ndivyo hasa ilivyotokea kwake, kwa kuwa
watu walimkanyaga langoni, naye akafa.

# 8

### *Ardhi ya Mshunami yarudishwa*

1 Basi Al-Yasa alikuwa amemwambia yule
mwanamke ambaye mwanawe alikuwa amefu-
fuliwa, "Ondoka wewe na jamaa yako ukaishi ma-
hali popote unapoweza kwa kitambo kidogo, kwa
sababu Mwenyezi Mungu ameamuru njaa katika
nchi hii ambayo itadumu kwa miaka saba."
2 Yule mwanamke akafanya kama vile yule
mtu wa Mungu alivyosema. Yeye na jamaa yake
wakaondoka na kwenda kuishi katika nchi ya
Wafilisti kwa miaka saba.
3 Baada ya miaka saba, yule mwanamke
akarudi kutoka nchi ya Wafilisti, akaenda kwa
mfalme kumsihi kwa ajili ya nyumba yake na
shamba lake.
4 Mfalme alikuwa anazungumza na Gehazi,
mtumishi wa mtu wa Mungu, naye alikuwa
amesema, "Hebu niambie mambo yote makuu
yaliyofanywa na Al-Yasa."
5 Gehazi alipokuwa akimweleza mfalme jinsi
Al-Yasa alivyomfufua mtu, yule mwanamke am-
baye mwanawe alikuwa amefufuliwa na Al-Yasa
akaja ili amsihi mfalme kwa ajili ya nyumba yake
na shamba lake.

Gehazi akasema, "Huyu ndiye huyo
mwanamke, bwana wangu mfalme, na huyu
ndiye mwanawe ambaye Al-Yasa alimfufua."
6 Mfalme akamuuliza yule mwanamke kuhusu
mambo hayo, naye akamweleza.

Ndipo akaamuru afisa amshughulikie, kwa kumwambia, “Mrudishie huyu mwanamke kila kitu kilichokuwa mali yake, pamoja na mapato yote yaliyotokana na shamba lake tangu siku alipoondoka nchini hadi sasa.”

### *Hazaeli amuua Ben-Hadadi*

7 Al-Yasa akaenda Dameski, naye Ben-Hadadi mfalme wa Aramu alikuwa mgonjwa. Mfalme alipoambiwa, “Mtu wa Mungu amekuja hadi hapa,”

8 mfalme akamwambia Hazaeli, “Chukua zawadi na uende kumlaki mtu wa Mungu. Muulize Mwenyezi Mungu kupitia yeye, kwamba, ‘Je, nitapona ugonjwa huu?’ ”

9 Hazaeli akaenda kumlaki Al-Yasa, akiwa amechukua zawadi ya kila kitu kizuri kilichopatikana Dameski, mizigo iliyobebwa na ngamia arobaini. Akaingia ndani na kusimama mbele yake, akasema, “Mwanao Ben-Hadadi mfalme wa Aramu amenituma niulize, ‘Je, nitapona ugonjwa huu?’ ”

10 Al-Yasa akajibu, “Nenda ukamwambie, ‘Hakika utapona’; lakini Mwenyezi Mungu amenifunulia kwamba kweli atakufa.”

11 Al-Yasa akamkazia Hazaeli macho kwa nguvu hata akaona aibu. Kisha mtu wa Mungu akaanza kulia.

12 Hazaeli akauliza “Kwa nini bwana wangu analia?”

Al-Yasa akajibu, “Kwa sababu najua mabaya utakayowatendea Waisraeli. Utachoma moto ngome zao, utawaua vijana wao kwa upanga,

kuwatupa chini kwa nguvu watoto wachanga, na kuwatumbua wanawake wenye mimba.”

13 Hazaeli akasema, “Itawezekanaje mtumishi wako, aliye mbwa tu, kufanya tendo la ajabu hivyo?”

Al-Yasa akamjibu, “Mwenyezi Mungu amenionesha kuwa utakuwa mfalme wa Aramu.”

14 Kisha Hazaeli akamwacha Al-Yasa na kumrudia bwana wake. Ben-Hadadi akamuuliza, “Al-Yasa alikuambia nini?” Hazaeli akajibu, “Aliniambia kwamba hakika utapona.”

15 Lakini kesho yake Hazaeli akachukua nguo nzito, akailoweka ndani ya maji, akaitandaza juu ya uso wa mfalme, hivyo akafa. Kisha Hazaeli akawa mfalme baada yake.

### *Yehoramu mfalme wa Yuda*
### *(2 Nyakati 21:1-20)*

16 Katika mwaka wa tano wa Yoramu mwana wa Ahabu mfalme wa Israeli, wakati huo Yehoshafati akiwa mfalme wa Yuda, Yehoramu mwana wa Yehoshafati akaanza kutawala kama mfalme wa Yuda.

17 Alikuwa na umri wa miaka thelathini na mbili alipoanza kutawala, naye akatawala huko Yerusalemu kwa miaka nane.

18 Akaenenda katika njia za wafalme wa Israeli, kama nyumba ya Ahabu ilivyokuwa imefanya, kwa kuwa alimwoa binti Ahabu. Akatenda maovu machoni pa Mwenyezi Mungu.

19 Hata hivyo, kwa ajili ya Daudi mtumishi wake, Mwenyezi Mungu hakutaka kuiangamiza Yuda. Alikuwa ameahidi kuidumisha taa kwa ajili ya Daudi na wazao wake milele.

20 Wakati wa utawala wa Yehoramu, Edomu
waliasi dhidi ya Yuda na kujiwekea mfalme wao
wenyewe.
21 Basi Yehoramu akaenda Sairi pamoja na
magari yake yote ya vita. Waedomu wakamzun-
guka yeye na majemadari wake wa magari yake
ya vita, lakini akaondoka, akapenya usiku na
kuwashambulia Waedomu. Hata hivyo, jeshi
lake likatorokea nyumbani mwao.
22 Hadi leo Edomu wameasi dhidi ya Yuda.
Libna pia wakaasi wakati huo huo.

23 Kuhusu matukio mengine ya utawala
wa Yehoramu na yote aliyoyafanya, je,
hayakuandikwa katika kitabu cha kumbukumbu
za wafalme wa Yuda?
24 Yehoramu akalala na baba zake, akazikwa
pamoja nao katika Mji wa Daudi. Naye Ahazia
mwanawe akawa mfalme baada yake.

### *Ahazia mfalme wa Yuda*
### *(2 Nyakati 22:1-6)*

25 Katika mwaka wa kumi na mbili wa utawala
wa Yoramu mwana wa Ahabu mfalme wa Israeli,
Ahazia mwana wa Yehoramu mfalme wa Yuda
alianza kutawala.
26 Ahazia alikuwa na umri wa miaka ishirini
na mbili alipoanza kutawala, naye akatawala
katika Yerusalemu kwa mwaka mmoja. Mama
yake aliitwa Athalia, mjukuu wa Omri mfalme
wa Israeli.
27 Akaenenda katika njia za nyumba ya
Ahabu, na kutenda maovu machoni pa Mwenyezi

Mungu, kama nyumba ya Ahabu ilivyokuwa imefanya, kwa kuwa alikuwa ameoa kutoka nyumba ya Ahabu.

28 Ahazia akaenda vitani na Yoramu mwana wa Ahabu kupigana na Hazaeli mfalme wa Aramu huko Ramoth-Gileadi. Waaramu wakamjeruhi Yoramu.
29 Hivyo Mfalme Yoramu akarudi Yezreeli ili apate kuuguza majeraha aliyojeruhiwa na Waaramu huko Ramothi* alipopigana na Hazaeli mfalme wa Aramu.

Ndipo Ahazia mwana wa Yehoramu mfalme wa Yuda akashuka kwenda Yezreeli kumtazama Yoramu mwana wa Ahabu, kwa sababu alikuwa amejeruhiwa.

# 9

## *Yehu atiwa mafuta kuwa Mfalme*

1 Nabii Al-Yasa akamwita mtu mmoja kutoka kwa wana wa manabii na kumwambia, “Jikaze viuno, uichukue hii chupa ya mafuta, na uende Ramoth-Gileadi.
2 Ukifika huko, mtafute Yehu mwana wa Yehoshafati, mwana wa Nimshi. Nenda kwake, umtenge na wenzake, na umpeleke katika chumba cha ndani.
3 Kisha chukua hii chupa na umimine mafuta juu ya kichwa chake, nawe utangaze, ‘Hivi ndivyo asemavyo Mwenyezi Mungu: Ninakupaka mafuta uwe mfalme juu ya Israeli.’ Kisha ufungue mlango na ukimbie; usikawie!”

---

* **8:29** *Rama* kwa Kiebrania

4 Basi yule kijana nabii akaenda Ramoth-Gileadi.
5 Alipofika, akawakuta maafisa wa jeshi wameketi pamoja, akasema, “Nina ujumbe wako, ee jemadari.”

Yehu akauliza, “Kwa yupi miongoni mwetu?”

Akamjibu, “Kwako wewe, jemadari.”

6 Yehu akainuka na kuingia ndani ya nyumba. Ndipo yule nabii akamimina mafuta juu ya kichwa cha Yehu, na kutangaza, “Hivi ndivyo asemavyo Mwenyezi Mungu, Mungu wa Israeli: ‘Ninakupaka mafuta uwe mfalme juu ya watu wa Mwenyezi Mungu, yaani Israeli.
7 Inakupasa uiangamize nyumba ya bwana wako Ahabu, nami nitalipiza kisasi cha damu ya watumishi wangu manabii na damu ya watumishi wote wa Mwenyezi Mungu iliyomwagwa na Yezebeli.
8 Nyumba yote ya Ahabu itaangamia. Nitamkatilia mbali kila mzaliwa wa kiume wa Ahabu katika Israeli, aliye mtumwa ama aliye huru.
9 Nitaifanya nyumba ya Ahabu kuwa kama ile nyumba ya Yeroboamu mwana wa Nebati, na kama ile nyumba ya Baasha mwana wa Ahiya.
10 Kuhusu Yezebeli, mbwa watamla kwenye kiwanja huko Yezreeli, wala hakuna mtu atakayemzika.’ ” Kisha akafungua mlango na kukimbia.

11 Yehu alipotoka nje na kurudi kwenda kwa maafisa wenzake, mmoja wao akamuuliza, “Je, kila kitu ni salama? Kwa nini huyu mwenye wazimu alikuja kwako?”

Yehu akajibu, “Wewe unamfahamu huyo mtu, na aina ya mambo ambayo yeye husema.”
12 Wakasema, “Hiyo siyo kweli! Tuambie.”

Yehu akasema, “Haya ndio aliyoniambia: ‘Hivi ndivyo asemavyo Mwenyezi Mungu: Ninakupaka mafuta uwe mfalme juu ya Israeli.’ ”
13 Wakaharakisha kuvua mavazi yao, na kuyatandaza chini ya Yehu ili akanyage juu kwenye ngazi ya nje. Kisha wakapiga tarumbeta na kupaza sauti wakisema, “Yehu ni mfalme!”

### *Yehu awaua Yoramu na Ahazia*

14 Basi Yehu mwana wa Yehoshafati, mwana wa Nimshi, akapanga njama dhidi ya Yoramu. (Wakati huu, Yoramu na Waisraeli wote walikuwa wakiilinda Ramoth-Gileadi dhidi ya Hazaeli mfalme wa Aramu,
15 lakini Mfalme Yoramu alikuwa amerudishwa Yezreeli ili kujiuguza kutokana na majeraha ambayo Waaramu walimtia katika vita na Hazaeli mfalme wa Aramu.) Yehu akasema, “Kama hii ndiyo nia yenu, msimruhusu hata mmoja kutoroka nje ya mji kwenda kupeleka habari huko Yezreeli.”
16 Ndipo Yehu akaingia katika gari lake la vita na kuendesha kwenda Yezreeli, kwa sababu Yoramu alikuwa amepumzika huko, na Ahazia mfalme wa Yuda alikuwa ameenda kumwona.
17 Mlinzi aliyesimama juu ya kinara cha Yezreeli alipoona askari wa Yehu wanakuja, akaita akisema, “Naona askari wanakuja.”

Yoramu akaamuru, “Mtwae mpanda farasi umtume akakutane nao na kuuliza, ‘Je, mmekuja kwa amani?’ ”

18 Mpanda farasi akaondoka kwenda kukutana
na Yehu na kusema, “Hivi ndivyo asemavyo
mfalme: ‘Je, mmekuja kwa amani?’ ”

Yehu akamjibu, “Una nini na amani? Unga msafara nyuma yangu.”

Mlinzi akatoa habari, “Mjumbe amewafikia lakini harudi.”

19 Basi mfalme akamtuma mpanda farasi wa
pili. Alipowafikia akasema, “Hivi ndivyo ase-
mavyo mfalme, ‘Je, mmekuja kwa amani?’ ”

Yehu akajibu, “Una nini na amani? Unga msafara nyuma yangu.”

20 Yule mlinzi akatoa taarifa akasema,
“Mjumbe amewafikia, lakini hata yeye harudi.
Uendeshaji ule ni kama wa Yehu mwana wa
Nimshi, anaendesha kama mwenye wazimu!”

21 Yoramu akaagiza, akasema, “Weka tayari
gari langu la vita.” Na baada ya gari kuwa tayari,
Yoramu mfalme wa Israeli, na Ahazia mfalme wa
Yuda, wakaondoka kila mmoja kwenye gari lake
ili kukutana na Yehu. Walikutana naye katika
shamba lililokuwa mali ya Nabothi, Myezreeli.

22 Yoramu alipomwona Yehu, akauliza, “Je,
Yehu, umekuja kwa amani?”

Yehu akajibu, “Kunawezaje kuwa na amani wakati ibada za sanamu na uchawi wa mama yako Yezebeli bado ziko?”

23 Yoramu akageuka nyuma na kukimbia,
akimwambia Ahazia, “Huu ni uhaini, Ahazia!”

24 Kisha Yehu akatwaa upinde wake na kum-
choma Yoramu katikati ya mabega. Mshale
ukapenya kwenye moyo wake, naye akaanguka
ghafula ndani ya gari lake la vita.

25 Yehu akamwambia Bidkari, mwendeshaji wa
gari lake la vita, “Mwinue na umtupe katika
shamba lililokuwa mali ya Nabothi, Myezreeli.
Kumbuka jinsi mimi na wewe tulivyokuwa
tukiendesha pamoja magari yetu ya vita nyuma
ya Ahabu baba yake, wakati Mwenyezi Mungu
alitoa unabii huu kumhusu:
26 ‘Jana niliona damu ya Nabothi na damu ya
wanawe, nami kwa hakika nitakufanya uilipe
juu ya shamba hili, asema Mwenyezi Mungu.’
Sasa basi, mwinue na umtupe juu ya kiwanja,
kulingana na neno la Mwenyezi Mungu.”

27 Ahazia mfalme wa Yuda alipoona kili-
chotokea, akakimbia kupitia barabara ya Beth-
Hagani. Yehu akamkimbiza akipaza sauti na
kusema, “Muue naye pia!” Wakamjeruhi katika
gari lake la vita kwenye njia inayoelekea Guri
karibu na Ibleamu, lakini akatorokea Megido,
akafia huko.
28 Watumishi wake wakambeba kwa gari
la vita na kumpeleka Yerusalemu, wakamzika
pamoja na baba zake kwenye kaburi lake katika
Mji wa Daudi.
29 (Katika mwaka wa kumi na moja wa Yoramu
mwana wa Ahabu, Ahazia alianza kutawala
katika Yuda.)

### *Yezebeli auawa*

30 Kisha Yehu akaenda Yezreeli. Yezebeli ali-
posikia habari hii, akayapaka macho yake wanja,
akatengeneza nywele zake na kutazama nje diris-
hani.

31 Yehu alipokuwa akiingia langoni, Yezebeli
akasema, “Je, umekuja kwa amani, Zimri, wewe
muuaji wa bwana wako?”
32 Yehu akaangalia juu dirishani na kuita, “Je, ni
nani aliye upande wangu? Ni nani?” Matowashi
wawili au watatu wakamtazama.
33 Yehu akasema, “Mtupeni huyo mwanamke
chini!” Kwa hiyo wakamtupa chini, nayo sehemu
ya damu yake ikatapanyika ukutani, na nyingine
juu ya farasi walipokuwa wakimkanyaga kwa
miguu yao.
34 Yehu akaingia ndani, akala na akanywa.
Akasema, “Mshughulikieni huyo mwanamke
aliyelaaniwa. Mzikeni, kwa sababu alikuwa binti
ya mfalme.”
35 Lakini walipotoka kwenda kumzika,
hawakukuta kitu chochote isipokuwa fuvu la
kichwa, miguu yake na mikono.
36 Wakarudi na kumwambia Yehu, ambaye
alisema, “Hili ndilo neno la Mwenyezi Mungu
alilosema kwa kinywa cha mtumishi wake Ilya
Mtishbi, kwamba: Katika kiwanja cha Yezreeli,
mbwa wataila nyama ya Yezebeli.
37 Maiti ya Yezebeli itakuwa kama kinyesi juu
ya ardhi katika uwanja wa Yezreeli, kwamba
hakutakuwa mtu atakayeweza kusema, ‘Huyu ni
Yezebeli.’ ”

# 10

*Jamii ya Ahabu wauawa*

1 Basi huko Samaria walikuwepo wana sabini
wa nyumba ya Ahabu. Kwa hiyo Yehu akaandika
barua na kuzituma Samaria: kwa maafisa wa

Yezreeli, kwa wazee, na kwa walezi wa watoto
wa Ahabu. Akasema,
2 "Mara tu barua hii itakapokufikia, kwa kuwa
wana wa bwana wako wapo pamoja nawe, nawe
una magari ya vita na farasi, mji wenye ngome
na silaha,
3 mchague mwenye uwezo zaidi kati ya wana
wa bwana wako, na umweke kwenye kiti cha
utawala cha baba yake. Kisha upigane kwa ajili
ya nyumba ya bwana wako."
4 Lakini wakaogopa sana na kusema, "Ikiwa
wafalme wawili hawakuweza kupambana na
Yehu, sisi tutawezaje?"
5 Basi msimamizi wa jumba la mfalme,
mtawala wa mji, na wazee na walezi wakatuma
ujumbe huu kwa Yehu: "Sisi tu watumishi
wako, na tutafanya kila kitu utakachosema.
Hatutamteuwa mtu yeyote kuwa mfalme. Wewe
fanya uonalo kuwa ni bora."
6 Kisha Yehu akawaandikia barua ya pili,
akisema, "Ikiwa ninyi mko upande wangu na
mtanitii mimi, twaeni vichwa vya wana wa
bwana wenu, na mnijie huku Yezreeli kesho
wakati kama huu."

Wakati huo wana sabini wa mfalme walikuwa
wakiishi pamoja na viongozi wa mji wa Samaria,
waliokuwa wakiwalea.
7 Hiyo barua ilipowafikia, watu hawa
wakawachukua wale wana sabini wa mfalme
na kuwachinja wote. Wakaweka vichwa vyao
ndani ya makapu na kumpelekea Yehu huko
Yezreeli.
8 Mjumbe alipofika, akamwambia Yehu,
"Wameleta vichwa vya wana wa mfalme."

Ndipo Yehu akaagiza, “Viwekeni malundo mawili katika ingilio la lango la mji hadi asubuhi.”
9 Kesho yake asubuhi, Yehu akatoka nje. Akasimama mbele ya watu wote na akasema, “Hamna hatia. Ni mimi niliyepanga njama dhidi ya bwana wangu na kumuua, lakini ni nani aliyewaua wote hawa?
10 Fahamuni basi kwamba, hakuna neno ambalo Mwenyezi Mungu amesema dhidi ya nyumba ya Ahabu ambalo halitatimia. Mwenyezi Mungu amefanya lile aliloahidi kupitia mtumishi wake Ilya.”
11 Hivyo Yehu akaua kila mtu huko Yezreeli aliyekuwa amebaki wa nyumba ya Ahabu, ikiwa ni pamoja na wakuu wake, rafiki zake wa karibu, na makuhani wake. Hakuacha yeyote anusurike.
12 Kisha Yehu akaondoka kuelekea Samaria. Alipokuwa njiani karibu na nyumba ya kukatia manyoya ya kondoo, yaani Beth-Ekedi ya wachunga kondoo,
13 Yehu akakutana na watu wa jamaa ya Ahazia mfalme wa Yuda, akauliza, “Ninyi ni nani?”

Wao wakasema, “Sisi ni jamaa ya Ahazia, nasi tumeshuka kuwasalimu jamaa ya mfalme na ya mama malkia.”
14 Yehu akaagiza, “Wakamateni wakiwa hai!” Kwa hiyo wakawachukua wakiwa hai, watu arobaini na wawili, na kuwachinja kando ya kisima cha Beth-Ekedi. Hakuacha yeyote anusurike.
15 Baada ya kuondoka hapo, alimkuta Yehonadabu mwana wa Rekabu, aliyekuwa akienda kumlaki. Yehu akamsalimu na kusema, “Je, moyo

wako ni mnyofu kwangu kama moyo wangu ulivyo kwako?”

Yehonadabu akajibu, “Ndiyo.”

Yehu akasema, “Kama ndivyo, nipe mkono wako.” Yeye akampa mkono, naye Yehu akampandisha kwenye gari lake la vita.

16 Yehu akasema, “Twende pamoja ukaone
wivu wangu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.”
Hivyo wakasafiri pamoja kwenye gari lake la
vita.
17 Yehu alipofika Samaria, akawaua wale wote
waliokuwa wamesalia wa jamaa ya Ahabu,
akawaangamiza, sawasawa na neno la Mwenyezi
Mungu alilosema kupitia Ilya.

*Watumishi wa Baali wauawa*

18 Kisha Yehu akawaleta watu wote pamoja na
kuwaambia, “Ahabu alimtumikia Baali kidogo.
Lakini Yehu atamtumikia zaidi.
19 Sasa waiteni manabii wote wa Baali,
watumishi wake wote na makuhani wake
wote. Hakikisheni kwamba hakuna hata
mmoja atakayekosekana, kwa sababu ninaenda
kutoa kafara kubwa sana kwa Baali. Yeyote
atakayeshindwa kuja hataendelea kuishi.”
Lakini Yehu alifanya hivyo kwa hila ili apate
kuwaangamiza watumishi wote wa Baali.
20 Yehu akasema, “Itisheni kusanyiko kwa hes-
hima ya Baali.” Basi wakatangaza jambo hilo.
21 Kisha Yehu akapeleka ujumbe katika Israeli
yote, nao watumishi wote wa Baali wakaja,
hakuna hata mmoja ambaye hakufika. Waka-
songamana ndani ya hekalu la Baali hadi likajaa
tangu mlango hadi mwisho wake.

22 Naye Yehu akamwambia yule aliyekuwa
mtunza chumba cha mavazi, “Leta majoho
kwa ajili ya watumishi wote wa Baali.” Basi
akawaletea majoho.

23 Kisha Yehu na Yehonadabu mwana wa Rek-
abu wakaingia ndani ya hekalu la Baali. Yehu
akawaambia watumishi wa Baali, “Tazameni kila
mahali mhakikishe kwamba hakuna hata mtu-
mishi mmoja wa Mwenyezi Mungu aliye hapa
pamoja nanyi, ila ni watumishi wa Baali tu.”
24 Kwa hiyo wakaingia ndani ili kutoa ka-
fara na sadaka ya kuteketezwa. Wakati huu,
Yehu alikuwa amewaweka watu wake themanini
akiwa amewapa onyo kwamba, “Ikiwa mmoja
wenu atamwachia mtu yeyote ninayemweka
mikononi mwenu atoroke, itakuwa uhai wako
kwa uhai wake.”

25 Mara baada ya Yehu kutoa sadaka ya
kuteketezwa, akawaamuru walinzi na maafisa:
“Ingieni ndani, waueni; asitoroke hata mmoja.”
Basi wakawakatakata kwa upanga. Walinzi na
maafisa wakazitupa zile maiti nje, kisha wakain-
gia mahali pa ndani pa ibada katika hekalu la
Baali.
26 Wakaileta ile nguzo ya kuabudiwa nje ya
hekalu la Baali, na wakaichoma moto.
27 Wakabomoa ile nguzo ya kuabudiwa ya Baali
pamoja na hekalu la Baali, nao watu waka-
pafanya kuwa choo hadi leo.

28 Kwa hiyo Yehu akaangamiza kuabudiwa kwa
Baali katika Israeli.
29 Hata hivyo, Yehu hakuziacha dhambi za
Yeroboamu mwana wa Nebati, ambazo alikuwa

amesababisha Israeli kuzitenda, yaani kuabudu
ndama za dhahabu huko Betheli ya Dani.
30 Mwenyezi Mungu akamwambia Yehu, “Kwa
kuwa umefanya vyema kwa kutimiza yaliyo
sawa machoni pangu, na umetenda kwa nyumba
ya Ahabu yale yote niliyokuwa nimekusudia
kutenda, wazao wako wataketi kwenye kiti cha
utawala cha Israeli hadi kizazi cha nne.”
31 Lakini Yehu hakuwa mwangalifu kushika
sheria za Mwenyezi Mungu, Mungu wa Israeli,
kwa moyo wake wote. Hakuziacha dhambi za
Yeroboamu, ambazo alikuwa amesababisha Is-
raeli kuzitenda.
32 Katika siku hizo, Mwenyezi Mungu akaanza
kupunguza ukubwa wa Israeli. Hazaeli
akawashinda Waisraeli sehemu zote za nchi
yao
33 mashariki mwa Yordani, katika nchi yote
ya Gileadi (eneo la Gadi, Reubeni na Manase),
kutoka Aroeri karibu na Bonde la Arnoni kupitia
Gileadi hadi Bashani.
34 Kuhusu matukio mengine ya utawala wa
Yehu, yote aliyofanya na mafanikio yake yote, je,
hayakuandikwa katika kitabu cha kumbukumbu
za wafalme wa Israeli?
35 Yehu akalala na baba zake, akazikwa huko
Samaria. Naye Yehoahazi mwanawe akawa
mfalme baada yake.
36 Muda Yehu aliotawala Israeli huko Samaria
ulikuwa miaka ishirini na nane.

# 11

*Athalia na Yoashi*
*(2 Nyakati 22:10–23:21)*

1 Athalia mamaye Ahazia alipoona kuwa
mwanawe amekufa, akainuka na kuangamiza
jamaa yote ya mfalme.
2 Lakini Yehosheba, binti ya Mfalme Yehoramu,
aliyekuwa pia dada yake Ahazia, akamtwaa
Yoashi mwana wa Ahazia kwa siri kutoka mion-
goni mwa wana wa mfalme waliokuwa karibu
kuuawa. Akamweka Yoashi pamoja na yaya
wake ndani ya chumba cha kulala na kumficha
humo ili Athalia asimwone; kwa hiyo hakuuawa.
3 Alibaki amefichwa pamoja na yaya wake
katika Hekalu la Mwenyezi Mungu kwa muda
wa miaka sita wakati Athalia alikuwa akitawala
nchi.
4 Katika mwaka wa saba, Yehoyada akatuma-
nia wakuu wa vikundi vya mamia, na Wakari*
na walinzi, nao wakaletwa kwake katika Hekalu
la Mwenyezi Mungu. Alifanya agano nao na
kuwaapisha katika Hekalu la Mwenyezi Mungu.
Ndipo akawaonesha mwana wa mfalme.
5 Akawaamuru akisema, “Hivi ndivyo iwa-
pasavyo kufanya: Ninyi ambao mko makundi
matatu mnaoingia zamu siku ya Sabato, theluthi
moja italinda jumba la kifalme,
6 theluthi nyingine Lango la Suri, na theluthi
nyingine lango lililo nyuma ya walinzi, ambao
hupeana zamu kulinda Hekalu.
7 Nanyi ambao mko katika makundi mengine
mawili ambao kwa kawaida hupumzika siku
ya Sabato, wote mtalinda Hekalu kwa ajili ya
mfalme.

---

* **11:4** yaani *Wakerethi* (taz. 1 Samweli 30:14; Ezekieli 25:16; Sefania 2:5, 6).

8 Jipangeni kumzunguka mfalme, kila mtu akiwa na silaha yake mkononi. Yeyote anayesogelea safu zenu lazima auawe. Kaeni karibu na mfalme popote aendapo.”

9 Wakuu wa vikosi vya mamia wakafanya vile kuhani Yehoyada aliagiza. Kila mmoja akawachukua watu wake, wale waliokuwa wakiingia zamu siku ya Sabato na wale waliokuwa wakienda mapumziko, nao wakaja kwa kuhani Yehoyada.

10 Ndipo akawapa wale wakuu mikuki na ngao zilizokuwa za Mfalme Daudi, zilizokuwa ndani ya Hekalu la Mwenyezi Mungu.

11 Wale walinzi, kila mmoja akiwa na silaha yake mkononi mwake, wakajipanga kumzunguka mfalme, karibu na madhabahu na Hekalu, kuanzia upande wa kusini hadi upande wa kaskazini mwa Hekalu.

12 Yehoyada akamtoa mwana wa mfalme na kumvika taji, akampa nakala ya agano, na kumtangaza kuwa mfalme. Wakampaka mafuta, nao watu wakapiga makofi na kupaza sauti, wakisema, “Mfalme aishi maisha marefu!”

13 Athalia aliposikia kelele za walinzi pamoja na watu, akawaendea watu katika Hekalu la Mwenyezi Mungu.

14 Akaangalia, na tazama, mfalme alikuwa amesimama karibu na nguzo, kama ilivyokuwa desturi. Maafisa na wapiga tarumbeta walikuwa kando ya mfalme, nao watu wote wa nchi walikuwa wanashangilia na kupiga tarumbeta. Ndipo Athalia akararua mavazi yake na kulia, “Uhaini! Uhaini!”

15 Kuhani Yehoyada akawaamuru majemadari
wa vikosi vya mamia, waliokuwa viongozi wa
jeshi, “Mtoeni nje kati ya safu, na mkamuue kwa
upanga yeyote anayemfuata.” Kwa kuwa kuhani
alikuwa amesema, “Hatauawa ndani ya Hekalu
la Mwenyezi Mungu.”
16 Basi wakamkamata Athalia alipofika mahali
farasi huingilia katika viwanja vya jumba la
mfalme, wakamuua hapo.

17 Kisha Yehoyada akafanya agano kati ya
Mwenyezi Mungu na mfalme na watu kwamba
watakuwa watu wa Mwenyezi Mungu. Akafanya
pia agano kati ya mfalme na watu.
18 Watu wote wa nchi wakaenda kwenye
hekalu la Baali na kulibomoa. Wakavunjavunja
madhabahu na sanamu, na kumuua Matani
kuhani wa Baali mbele ya hayo madhabahu.

Kisha Yehoyada kuhani akawaweka walinzi
kwenye Hekalu la Mwenyezi Mungu.
19 Pamoja naye akawachukua majemadari wa
mamia, Wakari, walinzi na watu wote wa nchi,
nao kwa pamoja wakamteremsha mfalme ku-
toka Hekalu la Mwenyezi Mungu na kwenda
kwenye jumba la mfalme, wakiingilia njia ya
lango la walinzi. Ndipo mfalme akachukua
nafasi yake kwenye kiti cha ufalme;
20 nao watu wote wa nchi wakafurahi. Mji
ukatulia, kwa sababu Athalia alikuwa ameuawa
kwa upanga nyumbani mwa mfalme.

21 Yoashi alikuwa na umri wa miaka saba
alipoanza kutawala.

# 12

### *Yoashi akarabati Hekalu*

1 Katika mwaka wa saba wa utawala wa Yehu, Yoashi alianza kutawala, naye akatawala huko Yerusalemu miaka arobaini. Mama yake aliitwa Sibia, kutoka Beer-Sheba.

2 Yoashi akafanya yaliyo mema machoni pa Mwenyezi Mungu miaka yote ambayo Yehoyada kuhani alikuwa akimwelekeza.

3 Hata hivyo mahali pa juu pa kuabudia hapakuondolewa. Watu waliendelea kutoa kafara na kufukiza uvumba huko.

4 Yoashi akawaambia makuhani, “Kusanyeni fedha zote zitakazoletwa kama sadaka takatifu kwenye Hekalu la Mwenyezi Mungu, yaani fedha zilizokusanywa watu walipohesabiwa, fedha zilizopokelewa kutokana na nadhiri za watu binafsi, na fedha zilizoletwa kwa hiari hekaluni.

5 Kila kuhani na apokee fedha kutoka kwa mmoja wa watunza hazina, nazo zitumike kukarabati uharibifu wowote unaoonekana katika Hekalu.”

6 Lakini ikawa kufikia mwaka wa ishirini na tatu wa utawala wake Mfalme Yoashi, makuhani walikuwa bado hawajalikarabati Hekalu.

7 Kwa hiyo Mfalme Yoashi akamwita Yehoyada kuhani na makuhani wengine, akawauliza, “Kwa nini hamtengenezi uharibifu uliofanyika hekaluni? Msichukue fedha zaidi kutoka kwa watunza hazina wenu kwa ajili ya matumizi yenu, lakini kuanzia sasa ni lazima fedha yote itumike kwa ajili ya kukarabati Hekalu.”

8 Makuhani wakakubali kuwa hawatakusanya
tena fedha kutoka kwa watu na kwamba
hawatakarabati Hekalu wenyewe.

9 Yehoyada kuhani akachukua kisanduku na
akatoboa tundu kwenye kifuniko chake. Akaki-
weka kando ya madhabahu upande wa kulia
unapoingia hekaluni mwa Mwenyezi Mungu.
Makuhani waliolinda ingilio wakaweka ndani ya
kisanduku fedha zote ambazo zililetwa katika
Hekalu la Mwenyezi Mungu.
10 Kila mara walipoona kuwa kuna kiasi
kikubwa cha fedha ndani ya kisanduku, mwan-
dishi wa mfalme na kuhani mkuu walikuja,
wakazihesabu fedha hizo zilizoletwa katika
Hekalu la Mwenyezi Mungu, na kuziweka katika
mifuko.
11 Walipothibitisha kiasi cha hizo fedha, wali-
wapa watu walioteuliwa kusimamia kazi katika
Hekalu. Kwa fedha hizo, wakawalipa wale
watu waliofanya kazi katika Hekalu la Mwenyezi
Mungu: maseremala na wajenzi,
12 waashi na wakata mawe. Walinunua mbao
na mawe ya kuchongwa kwa ajili ya ukara-
bati wa Hekalu la Mwenyezi Mungu, na kulipia
gharama nyingine zote za kulitengeneza.

13 Fedha zilizoletwa kwenye Hekalu hazikutu-
miwa kutengenezea masinia ya fedha, mikasi
ya kusawazishia tambi, mabakuli ya kunyuny-
izia, tarumbeta wala vyombo vingine vyovyote
vya dhahabu au fedha kwa ajili ya Hekalu la
Mwenyezi Mungu;
14 zililipwa kwa wafanyakazi, ambao walizitu-
mia kwa kukarabati Hekalu.

15 Wao hawakudai hesabu ya fedha kutoka kwa
wale waliowapa ili kuwalipa wafanyakazi, kwa
sababu walifanya kwa uaminifu wote.
16 Fedha zilizopatikana kutokana na sadaka za
hatia na sadaka za dhambi hazikuletwa katika
Hekalu la Mwenyezi Mungu; zilikuwa mali ya
makuhani.
17 Basi Hazaeli mfalme wa Aramu akapanda
kuishambulia Gathi, akaiteka. Kisha akageuka ili
kuishambulia Yerusalemu.
18 Lakini Yoashi mfalme wa Yuda akavichukua
vyombo vyote vitakatifu vilivyowekwa wakfu
na baba zake, yaani Yehoshafati, Yehoramu na
Ahazia, wafalme wa Yuda, na vyombo vyake vy-
ote ambavyo alikuwa ameviweka wakfu, pamoja
na dhahabu yote iliyokuwa katika hazina za
Hekalu la Mwenyezi Mungu na katika jumba la
kifalme; akazipeleka kwa Hazaeli mfalme wa
Aramu, ambaye hatimaye aliondoka Yerusalemu.
19 Kuhusu matukio mengine ya utawala wa
Yoashi na yote aliyoyafanya, je, hayakuandikwa
katika kitabu cha kumbukumbu za wafalme wa
Yuda?
20 Maafisa wake wakapanga njama dhidi yake,
nao wakamuua Yoashi huko Beth-Milo, kwenye
barabara inayoteremka kuelekea Sila.
21 Maafisa waliomuua walikuwa Yozabadi
mwana wa Shimeathi, na Yehozabadi mwana wa
Shomeri. Akafa na akazikwa na baba zake katika
Mji wa Daudi. Naye Amazia mwanawe akawa
mfalme baada yake.

# 13

*Yehoahazi mfalme wa Israeli*

1 Katika mwaka wa ishirini na tatu wa utawala wa Yoashi mwana wa Ahazia mfalme wa Yuda, Yehoahazi mwana wa Yehu alianza kutawala Israeli katika Samaria, naye akatawala miaka kumi na saba.
2 Akafanya maovu machoni pa Mwenyezi Mungu kwa kufuata dhambi za Yeroboamu mwana wa Nebati, ambazo alikuwa amesababisha Israeli kuzitenda, na wala hakuziacha.
3 Kwa hiyo hasira ya Mwenyezi Mungu ikawaka dhidi ya Israeli na kwa muda mrefu akawaweka chini ya utawala wa Hazaeli mfalme wa Aramu, na Ben-Hadadi mwanawe.
4 Ndipo Yehoahazi akamsihi Mwenyezi Mungu ampe rehema, naye Mwenyezi Mungu akamsikiliza, kwa maana aliona jinsi mfalme wa Aramu alivyokuwa akiwatesa Israeli vikali.
5 Mwenyezi Mungu akamtoa mwokozi kwa ajili ya Israeli, nao wakaokoka kutoka mamlaka ya Aramu. Hivyo Waisraeli wakaishi katika nyumba zao wenyewe kama ilivyokuwa hapo awali.
6 Lakini hawakuziacha dhambi za nyumba ya Yeroboamu, ambazo alisababisha Israeli kuzitenda, bali wakaendelea kuzitenda. Nguzo ya Ashera pia iliendelea kusimama katika Samaria.
7 Hapakubaki kitu chochote katika jeshi la Yehoahazi isipokuwa wapanda farasi hamsini, magari kumi ya vita na askari wa miguu elfu kumi, kwa kuwa mfalme wa Aramu alikuwa amewaangamiza hao wengine na kuwafanya kama mavumbi wakati wa kupura nafaka.
8 Kuhusu matukio mengine ya utawala wa Yehoahazi, yote aliyoyafanya na mafanikio yake,

je, hayakuandikwa katika kitabu cha kumbukumbu za wafalme wa Israeli?
9 Yehoahazi akalala na baba zake, akazikwa huko Samaria. Naye Yehoashi* mwanawe akawa mfalme baada yake.

### *Yehoashi mfalme wa Israeli*

10 Katika mwaka wa thelathini na saba wa utawala wa Yoashi mfalme wa Yuda, Yehoashi mwana wa Yehoahazi alianza kutawala Israeli huko Samaria, naye akatawala miaka kumi na sita.
11 Alifanya maovu machoni pa Mwenyezi Mungu, na hakuacha dhambi yoyote kati ya zile za Yeroboamu mwana wa Nebati ambazo alikuwa amesababisha Israeli kuzitenda, bali aliendelea kuzitenda.
12 Na kuhusu matukio mengine ya utawala wa Yehoashi, yote aliyoyafanya na mafanikio yake, pamoja na vita vyake dhidi ya Amazia mfalme wa Yuda, je, hayakuandikwa katika kitabu cha kumbukumbu za wafalme wa Israeli?
13 Yehoashi akalala na baba zake, naye Yeroboamu akawa mfalme baada yake. Yehoashi akazikwa Samaria na wafalme wa Israeli.
14 Wakati huu, Al-Yasa alikuwa anaugua ugonjwa ambao baadaye ulimuua. Yehoashi mfalme wa Israeli akashuka kwenda kumwona na kumlilia. Akalia, “Baba yangu! Baba yangu! Magari ya vita ya Israeli na wapanda farasi wake!”
15 Al-Yasa akasema, “Leta upinde na baadhi ya mishale,” naye mfalme akafanya hivyo.

* **13:9** au *Yoashi*

16 Al-Yasa akamwambia mfalme wa Israeli,
"Shika upinde mikononi mwako." Alipokwisha
kuuchukua, Al-Yasa akaweka mikono yake juu ya
mikono ya mfalme.
17 Al-Yasa akasema, "Fungua dirisha la
mashariki," naye akalifungua. Al-Yasa akasema,
"Piga mshale!" Naye akapiga mshale. Al-Yasa
akasema, "Mshale wa ushindi wa Mwenyezi
Mungu, mshale wa ushindi juu ya Aramu!
Utawaangamiza Waaramu kabisa huko Afeki."
18 Kisha akasema, "Chukua mishale," naye
mfalme akaichukua. Al-Yasa akamwambia, "Piga
ardhi kwa hiyo mishale." Akaipiga mara tatu,
halafu akaacha.
19 Mtu wa Mungu akamkasirikia na akasema,
"Ungepiga chini mara tano au sita, ndipo
ungeishinda Aramu na kuiangamiza kabisa.
Lakini sasa utaishinda mara tatu tu."
20 Al-Yasa akafa, nao wakamzika.

Vikosi vya Wamoabu vilikuwa vinashambulia nchi kwa vita kila mwaka wakati wa vuli.
21 Ikawa Waisraeli fulani walipokuwa
wanamzika mtu, ghafula wakaona kikosi cha
washambuliaji, basi wakaitupa ile maiti ya
yule mtu ndani ya kaburi la Al-Yasa. Ile maiti
ilipogusa mifupa ya Al-Yasa, yule mtu akafufuka
na kusimama kwa miguu yake.
22 Hazaeli mfalme wa Aramu aliwatesa Israeli
wakati wote wa utawala wa Yehoahazi.
23 Lakini Mwenyezi Mungu akawarehemu na
akawahurumia, akaonesha kujishughulisha nao
kwa sababu ya agano lake na Ibrahimu, Isaka
na Yakobo. Hadi leo, hajawaangamiza wala
kuwafukuza mbele zake.

24 Hazaeli mfalme wa Shamu akafa, naye Ben-
Hadadi mwanawe akawa mfalme baada yake.
25 Kisha Yehoashi mwana wa Yehoahazi
akateka tena kutoka kwa Ben-Hadadi mwana wa Hazaeli ile miji aliyokuwa ameitwaa kwa vita kutoka kwa baba yake Yehoahazi. Yehoashi alimshinda mara tatu, hivyo akaweza kuiteka tena ile miji ya Waisraeli.

# 14

### *Amazia mfalme wa Yuda (2 Nyakati 25)*

1 Katika mwaka wa pili wa utawala wa
Yehoashi mwana wa Yehoahazi mfalme wa Israeli, Amazia mwana wa Yoashi mfalme wa Yuda alianza kutawala.
2 Alikuwa na umri wa miaka ishirini na
tano alipoanza kutawala, naye akatawala huko Yerusalemu kwa miaka ishirini na tisa. Mama yake aliitwa Yehoadani, kutoka Yerusalemu.
3 Akatenda yaliyo mema machoni pa Mwenyezi
Mungu, lakini sio kama Daudi baba yake alivyokuwa amefanya. Katika kila kitu alifuata mfano wa Yoashi baba yake.

4 Hata hivyo mahali pa juu pa kuabudia ha-
pakuondolewa. Watu waliendelea kutoa kafara na kufukiza uvumba huko.
5 Baada ya ufalme kuimarika mkononi mwake,
aliwaua maafisa waliomuua mfalme baba yake.
6 Hata hivyo, hakuwaua wana wa wale wauaji,
sawasawa na ilivyoandikwa katika Kitabu cha

Torati ya Musa, ambako Mwenyezi Mungu aliamuru, “Baba hawatauawa kwa ajili ya watoto wao, wala watoto kwa ajili ya baba zao. Kila mmoja atakufa kwa ajili ya dhambi zake mwenyewe.”

7 Ndiye aliwashinda Waedomu elfu kumi katika Bonde la Chumvi, na akauteka Sela katika vita, naye akauita Yoktheeli, jina ambalo mji huo unalo hadi leo.

8 Kisha Amazia akatuma wajumbe kwa Yehoashi mwana wa Yehoahazi, mwana wa Yehu, mfalme wa Israeli, akisema, “Njoo, tukabiliane uso kwa uso.”

9 Lakini Yehoashi mfalme wa Israeli akamjibu Amazia mfalme wa Yuda: “Mbaruti uliokuwa Lebanoni ulituma ujumbe kwa mwerezi uliokuwa Lebanoni, ‘Mtoe binti yako aolewe na mwanangu.’ Kisha mnyama wa mwituni aliyekuwa Lebanoni akaja na kuukanyaga ule mbaruti.

10 Hakika umeishinda Edomu, na sasa unajivuna. Jisifu katika ushindi wako, lakini kaa nyumbani mwako! Kwa nini unachokoza na kujiletea anguko lako mwenyewe na la Yuda pia?”

11 Hata hivyo, Amazia hakusikia, hivyo Yehoashi mfalme wa Israeli akashambulia. Yeye na Amazia mfalme wa Yuda wakakutana uso kwa uso huko Beth-Shemeshi katika Yuda.

12 Yuda ikashindwa na Israeli, na kila mtu akakimbilia nyumbani mwake.

13 Yehoashi mfalme wa Israeli akamteka Amazia mfalme wa Yuda, mwana wa Yoashi, mwana wa Ahazia, huko Beth-Shemeshi. Kisha

Yehoashi akaenda Yerusalemu na kuubomoa ukuta wa Yerusalemu kuanzia Lango la Efraimu hadi Lango la Pembeni, sehemu yenye urefu wa kama dhiraa mia nne*.
14 Akachukua dhahabu yote na fedha na vyombo vyote vilivyopatikana ndani ya Hekalu la Mwenyezi Mungu na katika hazina zote za jumba la mfalme. Akachukua pia mateka na akarudi Samaria.
15 Kuhusu matukio mengine ya utawala wa Yehoashi, aliyoyafanya na mafanikio yake, pamoja na vita vyake dhidi ya Amazia mfalme wa Yuda, je, hayakuandikwa katika kitabu cha kumbukumbu za wafalme wa Israeli?
16 Yehoashi akalala na baba zake, akazikwa Samaria na wafalme wa Israeli. Naye Yeroboamu mwanawe akawa mfalme baada yake.
17 Amazia mwana wa Yoashi mfalme wa Yuda aliishi miaka kumi na tano baada ya kifo cha Yehoashi mwana wa Yehoahazi mfalme wa Israeli.
18 Kuhusu matukio mengine ya utawala wa Amazia, je, hayakuandikwa katika kitabu cha kumbukumbu za wafalme wa Yuda?
19 Wakapanga njama dhidi ya Amazia huko Yerusalemu, naye akakimbilia Lakishi, lakini wakawatuma watu wamfuatilie huko Lakishi, nao wakamuua huko.
20 Akarudishwa kwa farasi, akazikwa huko Yerusalemu pamoja na baba zake katika Mji wa Daudi.
21 Kisha watu wote wa Yuda wakamchukua Azaria† aliyekuwa na umri wa miaka kumi na

* **14:13** Dhiraa 400 ni sawa na mita 180. † **14:21** au *Uzia*

sita, na kumfanya mfalme mahali pa Amazia
baba yake.
22 Ndiye aliijenga upya Elathi na kuirudisha
kwa Yuda baada ya Amazia kulala na baba zake.

### *Yeroboamu wa pili mfalme wa Israeli*

23 Katika mwaka wa kumi na tano wa utawala
wa Amazia mwana wa Yoashi mfalme wa Yuda,
Yeroboamu mwana wa Yehoashi mfalme wa
Israeli alianza kutawala huko Samaria, naye
akatawala kwa miaka arobaini na moja.
24 Akafanya maovu machoni pa Mwenyezi
Mungu, na hakuacha dhambi hata moja ya Yer-
oboamu mwana wa Nebati, ambazo alikuwa
amesababisha Israeli kuzitenda.
25 Ndiye alirudishia mipaka ya Israeli kuanzia
Lebo-Hamathi hadi Bahari ya Araba, sawasawa
na neno la Mwenyezi Mungu, Mungu wa Israeli,
lililosemwa kupitia mtumishi wake Yona mwana
wa Amitai, nabii kutoka Gath-Heferi.
26 Mwenyezi Mungu alikuwa ameona jinsi kila
mmoja katika Israeli, awe mtumwa au aliye
huru, alivyoteseka kwa uchungu; hapakuwa na
yeyote wa kuwasaidia.
27 Kwa kuwa Mwenyezi Mungu alikuwa ha-
jasema kuwa atafuta jina la Israeli chini ya
mbingu, akawaokoa kwa mkono wa Yeroboamu
mwana wa Yehoashi.
28 Kuhusu matukio mengine ya utawala wa
Yeroboamu, yote aliyoyafanya na mafanikio yake
ya kijeshi, ikiwa ni pamoja na jinsi alivyorud-
isha Dameski na Hamathi kwa Israeli, ambayo
ilikuwa mali ya Yuda, je, hayakuandikwa katika
kitabu cha kumbukumbu za wafalme wa Israeli?

29 Yeroboamu akalala na baba zake, wafalme
wa Israeli. Naye Zekaria mwanawe akawa
mfalme baada yake.

# 15

### *Azaria mfalme wa Yuda*
### *(2 Nyakati 26)*

1 Katika mwaka wa ishirini na saba wa utawala
wa Yeroboamu mfalme wa Israeli, Azaria mwana
wa Amazia mfalme wa Yuda alianza kutawala.
2 Alikuwa na umri wa miaka kumi na sita
alipoanza kutawala, naye akatawala huko
Yerusalemu kwa miaka hamsini na mbili. Mama
yake aliitwa Yekolia, kutoka Yerusalemu.
3 Akatenda yaliyo mema machoni pa Mwenyezi
Mungu, kama Amazia baba yake alivyofanya.
4 Hata hivyo, mahali pa juu pa kuabudia ha-
pakuondolewa. Watu waliendelea kutoa kafara
na kufukiza uvumba huko.
5 Mwenyezi Mungu akampiga mfalme kwa
ukoma hadi siku aliyokufa, naye aliishi katika
nyumba iliyotengwa peke yake. Yothamu mwana
wa mfalme akawa msimamizi wa jumba la
mfalme, na akawatawala watu wa nchi.
6 Kuhusu matukio mengine ya utawala wa
Azaria na yote aliyoyafanya, je, hayakuandikwa
katika kitabu cha kumbukumbu za wafalme wa
Yuda?
7 Azaria akalala na baba zake, naye akazikwa
karibu nao katika Mji wa Daudi. Naye Yothamu
mwanawe akawa mfalme baada yake.

### *Zekaria mfalme wa Israeli*

8 Katika mwaka wa thelathini na nane wa
utawala wa Azaria mfalme wa Yuda, Zekaria
mwana wa Yeroboamu akawa mfalme wa Israeli
katika Samaria, naye akatawala miezi sita.
9 Akafanya maovu machoni pa Mwenyezi
Mungu, kama baba zake walivyofanya. Hakuzi-
acha dhambi za Yeroboamu mwana wa Nebati
ambazo alisababisha Israeli kuzitenda.
10 Shalumu mwana wa Yabeshi akapanga
njama dhidi ya Zekaria. Akamshambulia mbele
ya watu, akamuua, na akawa mfalme baada
yake.
11 Matukio mengine ya utawala wa Zekaria
yameandikwa kwenye kitabu cha kumbukumbu
za wafalme wa Israeli.
12 Kwa hiyo neno la Mwenyezi Mungu lililo-
nenwa kwa Yehu likatimia, kwamba, “Wazao
wako wataketi kwenye kiti cha utawala cha Is-
raeli hadi kizazi cha nne.”

### *Shalumu mfalme wa Israeli*

13 Shalumu mwana wa Yabeshi akawa mfalme
katika mwaka wa thelathini na tisa wa Uzia
mfalme wa Yuda, naye akatawala katika Samaria
kwa mwezi mmoja.
14 Kisha Menahemu mwana wa Gadi akaenda
kutoka Tirsa hadi Samaria. Akamshambulia
Shalumu mwana wa Yabeshi huko Samaria, aka-
muua, na akawa mfalme baada yake.
15 Matukio mengine ya utawala wa Shalumu,
na njama alizozipanga, yameandikwa katika
kitabu cha kumbukumbu za wafalme wa Israeli.
16 Wakati ule, akianzia Tirsa, Menahemu al-
ishambulia Tifsa na kila mtu ndani yake, na wale
waliokuwa maeneo jirani, kwa sababu walikataa

kufungua malango yao. Akaiangamiza Tifsa yote,
na kuwapasua tumbo wanawake wote wenye
mimba.

*Menahemu mfalme wa Israeli*

17 Katika mwaka wa thelathini na tisa wa
utawala wa Azaria mfalme wa Yuda, Mena-
hemu mwana wa Gadi akawa mfalme wa Israeli,
akatawala huko Samaria kwa miaka kumi.
18 Akatenda maovu machoni pa Mwenyezi
Mungu. Katika wakati wa utawala wake wote,
hakuziacha dhambi za Yeroboamu mwana wa
Nebati ambazo alisababisha Israeli kuzitenda.
19 Kisha Pulu mfalme wa Ashuru akaisham-
bulia Israeli. Menahemu mfalme wa Israeli
akampa talanta elfu moja* za fedha ili amsaidie
na kumwezesha katika utawala wake.
20 Menahemu akatoza fedha hizi kwa nguvu
kutoka kwa Israeli. Kila mtu tajiri alilaz-
imika kuchanga shekeli hamsini† za fedha am-
bazo alipewa mfalme wa Ashuru. Basi mfalme
wa Ashuru akajiondoa na hakuendelea kuikalia
nchi.
21 Kuhusu matukio mengine ya utawala
wa Menahemu na yote aliyoyafanya, je,
hayakuandikwa katika kitabu cha kumbukumbu
za wafalme wa Israeli?
22 Menahemu akalala na baba zake. Naye
Pekahia mwanawe akawa mfalme baada yake.

*Pekahia mfalme wa Israeli*

23 Katika mwaka wa hamsini wa utawala
wa Azaria mfalme wa Yuda, Pekahia mwana

---

* **15:19** Talanta 1,000 ni sawa na tani 34. † **15:20** Shekeli 50 ni sawa na gramu 600.

wa Menahemu akawa mfalme wa Israeli huko Samaria, akatawala miaka miwili.
24 Pekahia akafanya uovu machoni pa
Mwenyezi Mungu. Hakuziacha dhambi za Yeroboamu mwana wa Nebati, ambazo alisababisha Israeli kuzitenda.
25 Mmoja wa maafisa wake wakuu, Peka
mwana wa Remalia, akapanga njama dhidi yake. Akachukua watu hamsini wa Gileadi pamoja naye, akamuua Pekahia, pamoja na Argobu na Aria, katika ngome ya jumba la kifalme huko Samaria. Kwa hiyo Peka akamuua Pekahia, naye akawa mfalme baada yake.
26 Matukio mengine ya utawala wa Pekahia
na yote aliyoyafanya yameandikwa katika kitabu cha kumbukumbu za wafalme wa Israeli.

### *Peka mfalme wa Israeli*

27 Katika mwaka wa hamsini na mbili wa
utawala wa Azaria mfalme wa Yuda, Peka mwana wa Remalia akawa mfalme wa Israeli huko Samaria, naye alitawala miaka ishirini.
28 Akafanya maovu machoni pa Mwenyezi
Mungu. Hakuziacha dhambi za Yeroboamu mwana wa Nebati, ambazo alisababisha Israeli kuzitenda.
29 Wakati wa utawala wa Peka mfalme wa
Israeli, Tiglath-Pileseri mfalme wa Ashuru alikuja na kuteka Iyoni, Abel-Beth-Maaka, Yanoa, Kedeshi na Hazori. Akateka miji ya Gileadi na Galilaya, pamoja na nchi yote ya Naftali, na kuwahamishia watu wote Ashuru.
30 Kisha Hoshea mwana wa Ela akapanga
njama dhidi ya Peka mwana wa Remalia. Hoshea akamshambulia Peka na kumuua, kisha akawa

mfalme baada yake katika mwaka wa ishirini wa
Yothamu mwana wa Uzia.
31 Kuhusu matukio mengine ya utawala wa
Peka na yote aliyoyafanya, je, hayakuandikwa
katika kitabu cha kumbukumbu za wafalme wa
Israeli?

### *Yothamu mfalme wa Yuda*
### *(2 Nyakati 27)*

32 Katika mwaka wa pili wa utawala wa
Peka mwana wa Remalia mfalme wa Israeli,
Yothamu mwana wa Uzia mfalme wa Yuda
alianza kutawala.
33 Alikuwa na umri wa miaka ishirini na
tano alipoanza kutawala, naye akatawala huko
Yerusalemu miaka kumi na sita. Mama yake
aliitwa Yerusha binti Sadoki.
34 Akafanya yaliyo mema machoni pa
Mwenyezi Mungu, kama Uzia baba yake
alivyokuwa amefanya.
35 Hata hivyo, mahali pa juu pa kuabudia ha-
pakuondolewa. Watu waliendelea kutoa kafara
na kufukiza uvumba huko. Yothamu akajenga
upya Lango la Juu la Hekalu la Mwenyezi Mungu.
36 Kuhusu matukio mengine ya utawala
wa Yothamu na yale aliyoyafanya, je,
hayakuandikwa katika kitabu cha kumbukumbu
za wafalme wa Yuda?
37 (Katika siku hizo, Mwenyezi Mungu akaanza
kuwatuma Resini mfalme wa Aramu na Peka
mwana wa Remalia dhidi ya Yuda.)
38 Yothamu akalala na baba zake, akazikwa
pamoja nao katika Mji wa Daudi, mji wa baba
zake. Naye Ahazi mwanawe akawa mfalme
baada yake.

# 16

### *Ahazi mfalme wa Yuda*
### *(2 Nyakati 28)*

1 Katika mwaka wa kumi na saba wa utawala
wa Peka mwana wa Remalia, Ahazi mwana wa
Yothamu mfalme wa Yuda alianza kutawala.
2 Ahazi alikuwa na umri wa miaka ishirini
alipoanza kutawala, akatawala huko Yerusalemu
kwa miaka kumi na sita. Tofauti na Daudi
baba yake, hakufanya yaliyo mema machoni pa
Mwenyezi Mungu, Mungu wake.
3 Akaenenda katika njia za wafalme wa Israeli,
na hata akamtoa kafara mwanawe katika moto,
akifuata njia za machukizo za mataifa ambayo
Mwenyezi Mungu alikuwa ameyafukuza mbele
ya Waisraeli.
4 Akatoa sadaka na kufukiza uvumba katika
mahali pa juu pa kuabudia, juu ya vilima, na
chini ya kila mti uliotanda.
5 Kisha Resini mfalme wa Aramu na Peka
mwana wa Remalia mfalme wa Israeli wakaondoka kwenda kupigana dhidi ya Yerusalemu na
kumzingira Ahazi kwa jeshi, lakini hawakuweza
kumshinda.
6 Wakati ule, Resini mfalme wa Aramu akaurudisha mji wa Elathi kwa Aramu kwa kuwafukuza watu wa Yuda. Kisha Waedomu wakahamia Elathi, nao wanaishi huko hadi leo.
7 Ahazi akatuma wajumbe kumwambia
Tiglath-Pileseri mfalme wa Ashuru kwamba,
“Mimi ni mtumishi na mtumwa wako. Njoo
na uniokoe kutoka mkononi mwa mfalme
wa Aramu na wa mfalme wa Israeli, ambao
wananishambulia.”

8 Naye Ahazi akachukua fedha na dhahabu
zilizopatikana ndani ya Hekalu la Mwenyezi
Mungu na katika hazina ya jumba la mfalme, na
kuzituma kama zawadi kwa mfalme wa Ashuru.
9 Mfalme wa Ashuru akamwitikia kwa kusham-
bulia Dameski na kuiteka. Akawahamishia
wenyeji wake huko Kiri, na kumuua Resini.

10 Kisha Mfalme Ahazi akaenda Dameski kuku-
tana na Tiglath-Pileseri wa Ashuru. Akaona mad-
habahu huko Dameski, naye akamtumia Uria
kuhani mchoro wa hayo madhabahu, pamoja na
maelezo ya mpango kamili wa ujenzi wake.
11 Kwa hiyo Uria kuhani akajenga madhabahu
kulingana na mipango yote ambayo Mfalme
Ahazi alikuwa ameituma kutoka Dameski, na
akamaliza ujenzi kabla ya Mfalme Ahazi kurudi.
12 Mfalme aliporudi kutoka Dameski na kuona
hayo madhabahu, akayasogelea na kutoa sadaka
juu yake.
13 Akatoa sadaka yake ya kuteketezwa na
sadaka ya nafaka, akamimina sadaka ya kinywaji
na kunyunyizia damu ya sadaka zake za amani
juu ya hayo madhabahu.
14 Mfalme Ahazi akayaondoa madhabahu ya
zamani ya shaba kutoka hapo mbele ya Hekalu la
Mwenyezi Mungu, yaliyokuwa yamesimama kati
ya ingilio la Hekalu na hayo madhabahu mapya,
naye akayaweka upande wa kaskazini mwa hayo
madhabahu mapya.

15 Ndipo Mfalme Ahazi akatoa amri zifu-
atazo kwa Uria kuhani: "Juu ya hayo mad-
habahu kubwa mapya, toa sadaka ya asubuhi
ya kuteketezwa na sadaka ya jioni ya nafaka,

sadaka ya mfalme ya kuteketezwa pamoja na sadaka yake ya nafaka, sadaka ya kuteketezwa ya watu wote wa nchi, pamoja na sadaka yao ya nafaka na sadaka yao ya kinywaji. Unyunyize juu ya hayo madhabahu damu yote ya sadaka za kuteketezwa na dhabihu. Lakini mimi nitatumia hayo madhabahu ya zamani ya shaba kwa ajili ya kutafuta uongozi."

16 Naye Uria kuhani akafanya kama Mfalme Ahazi alivyoagiza.

17 Mfalme Ahazi akaondoa mbao za pembeni na kuondoa masinia kwenye vile vishikilio vilivyohamishika. Akaondoa ile Bahari kutoka mafahali wa shaba walioishikilia, na kuiweka kwenye kitako cha jiwe.

18 Kwa heshima ya mfalme wa Ashuru, akaliondoa pia pazia la Sabato lililokuwa limewekwa ndani ya Hekalu, na akaondoa ile njia ya kifalme ya kuingia kwenye Hekalu la Mwenyezi Mungu.

19 Kuhusu matukio mengine ya utawala wa Ahazi na yale aliyoyafanya, je, hayakuandikwa katika kitabu cha kumbukumbu za wafalme wa Yuda?

20 Ahazi akalala na baba zake, naye akazikwa pamoja nao katika Mji wa Daudi. Naye Hezekia mwanawe akawa mfalme baada yake.

# 17

### *Hoshea, mfalme wa mwisho wa Israeli*

1 Katika mwaka wa kumi na mbili wa utawala wa Ahazi mfalme wa Yuda, Hoshea mwana wa Ela akawa mfalme wa Israeli katika Samaria, naye akatawala miaka tisa.

2 Akafanya maovu machoni pa Mwenyezi Mungu, lakini si kama wafalme wengine wa Israeli waliomtangulia.

3 Mfalme Shalmanesa wa Ashuru akaenda na kumshambulia Mfalme Hoshea, ambaye hapo awali alikuwa akimlipa ushuru kwa sababu alikuwa mtumishi wake.

4 Lakini mfalme wa Ashuru akagundua kuwa Hoshea alikuwa msaliti, kwa kuwa alikuwa ame-
tuma wajumbe kwa So mfalme wa Misri. Wala
hakuendelea kulipa ushuru kwa mfalme wa Ashuru tena kama alivyokuwa anafanya kila mwaka. Kwa hiyo Shalmanesa akamkamata na kumfunga gerezani.

5 Mfalme wa Ashuru akaishambulia nchi yote, akapigana dhidi ya Samaria na kuuzingira kwa miaka mitatu.

## *Israeli kutekwa kwa sababu ya dhambi*

6 Katika mwaka wa tisa wa Hoshea, mfalme wa Ashuru akaiteka Samaria na kuwahamishia Waisraeli huko Ashuru. Akawakalisha huko Hala, na Gozani karibu na Mto Habori, na katika miji ya Wamedi.

7 Yote haya yalitukia kwa sababu Waisraeli walikuwa wametenda dhambi dhidi ya Mwenyezi Mungu, Mungu wao, aliyekuwa amewapandisha kutoka Misri akiwatoa chini ya utawala wa nguvu wa Farao mfalme wa Misri. Waliabudu miungu mingine,

8 na kufuata desturi za mataifa ambayo Mwenyezi Mungu alikuwa ameyafukuza mbele yao, pamoja na desturi ambazo wafalme wa Israeli walizileta.

9 Waisraeli wakafanya vitu kwa siri dhidi
ya Mwenyezi Mungu, Mungu wao, ambavyo
havikuwa sawa. Kuanzia kwenye mnara wa
ulinzi hadi kwenye mji wenye ngome, waliji-
jengea mahali pa juu pa kuabudia miungu katika
miji yao yote.
10 Wakaweka mawe ya kuabudiwa na nguzo za
Ashera juu ya kila kilima kirefu na chini ya kila
mti uliotanda.
11 Wakafukiza uvumba kila mahali pa juu pa
kuabudia, kama yalivyofanya yale mataifa am-
bayo Mwenyezi Mungu alikuwa ameyafukuza
mbele yao. Wakafanya mambo maovu ambayo
yalimghadhibisha Mwenyezi Mungu.
12 Wakatumikia sanamu, ingawa Mwenyezi
Mungu alikuwa amesema, “Msifanye mambo
haya.”
13 Mwenyezi Mungu akawaonya Israeli na
Yuda kupitia kwa manabii na waonaji wake
wote: “Acheni njia zenu mbaya. Shikeni amri
na maagizo yangu, kufuatana na Torati yangu
yote niliyowaagiza baba zenu kuitii, na ambayo
niliileta kwenu kupitia kwa watumishi wangu,
manabii.”
14 Lakini hawakusikiliza, walikuwa na shingo
ngumu kama baba zao, ambao hawakumwamini
Mwenyezi Mungu, Mungu wao.
15 Walizikataa amri zake, na agano alilolifanya
na baba zao, na maonyo aliyokuwa amewapa.
Wakafuata sanamu batili, nao wenyewe wakawa
batili. Wakayaiga mataifa yaliyowazunguka,
ingawa Mwenyezi Mungu alikuwa amewaonya
akiwaambia, “Msifanye kama wanavyofanya.”

16 Wakayaacha maagizo yote ya Mwenyezi
Mungu, Mungu wao, na kujitengenezea sanamu
mbili, walizozisubu katika sura ya ndama na
nguzo ya Ashera. Wakasujudia mianga yote ya
angani, na wakamtumikia Baali.
17 Wakawatoa kafara watoto wao wa kiume
na wa kike katika moto. Wakafanya uaguzi
na uchawi, nao wakajiuza wenyewe katika
kutenda uovu machoni pa Mwenyezi Mungu,
wakamghadhibisha.

18 Basi Mwenyezi Mungu akawakasirikia sana
Israeli na kuwaondoa kwenye uwepo wake. Ni
kabila la Yuda tu lililobaki.
19 Hata hivyo, Yuda nao hawakuzishika amri za
Mwenyezi Mungu, Mungu wao. Wakafuata des-
turi ambazo Israeli walikuwa wamezianzisha.
20 Kwa hiyo Mwenyezi Mungu aliwakataa watu
wote wa Israeli; akawatesa na kuwaachia katika
mikono ya wateka nyara hadi alipowaondoa
kwenye uwepo wake.

21 Alipokwisha kuwatenga Israeli mbali na
nyumba ya Daudi, wakamfanya Yeroboamu
mwana wa Nebati kuwa mfalme wao. Yer-
oboamu akawashawishi Israeli waache kumfu-
ata Mwenyezi Mungu na akawasababisha ku-
tenda dhambi kuu.
22 Nao Israeli wakadumu katika dhambi zote
za Yeroboamu mwana wa Nebati, nao hawakuzi-
acha
23 hadi Mwenyezi Mungu alipowaondoa
kwenye uwepo wake, kama vile alivyokuwa
ameonya kupitia watumishi wake wote manabii.
Hivyo watu wa Israeli wakaondolewa kutoka

nchi yao kwenda uhamishoni Ashuru, nao wako huko hata leo.

### *Samaria inakaliwa tena*

24 Mfalme wa Ashuru akawaleta watu kutoka Babeli, Kutha, Ava, Hamathi na Sefarvaimu na kuwaweka katika miji ya Samaria badala ya Waisraeli. Wakaimiliki Samaria na kuishi katika miji yake.

25 Wakati walianza kuishi humo, hawakumwabudu Mwenyezi Mungu, kwa hiyo akatuma simba miongoni mwao, wakawaua baadhi ya watu.

26 Habari ikapelekwa kwa mfalme wa Ashuru, kusema: "Watu uliowahamisha na kuwaweka katika miji ya Samaria hawajui kile Mungu wa nchi hiyo anachokitaka. Ametuma simba miongoni mwao, ambao wanawaua, kwa sababu watu hawajui anachokitaka."

27 Ndipo mfalme wa Ashuru akaamuru hivi: "Mtwae mmoja wa makuhani uliowachukua mateka kutoka Samaria ili arudi kuishi humo na awafundishe watu kile ambacho Mungu wa nchi anataka."

28 Basi mmoja wa makuhani aliyekuwa amepelekwa uhamishoni kutoka Samaria akaja kuishi Betheli, akawafundisha jinsi ya kumwabudu Mwenyezi Mungu.

29 Hata hivyo, kila kikundi cha taifa lililoletwa Samaria kilitengeneza miungu yao wenyewe katika miji kadhaa mahali walipoishi, nao wakaiweka katika nyumba za ibada za sanamu ambazo watu wa Samaria walikuwa wametengeneza katika mahali pa juu pa kuabudia.

30 Watu kutoka Babeli wakatengeneza Sukoth-
Benothi kuwa mungu wao, watu kutoka Kutha
wakatengeneza Nergali, na watu kutoka Hamathi
wakatengeneza Ashima;
31 Waavi wakatengeneza Nibhazi na Tartaki,
nao Wasefarvi wakachoma watoto wao kama
kafara kwa Adrameleki na Anameleki, miungu ya
Sefarvaimu.
32 Walimwabudu Mwenyezi Mungu, lakini pia
waliteua aina zote za watu wao ili kuwawakilisha
kama makuhani katika mahali pa ibada kwenye
mahali pa juu pa kuabudia.
33 Walimwabudu Mwenyezi Mungu, lakini pia
waliitumikia miungu yao kulingana na desturi za
mataifa walikotoka.
34 Hadi leo wanashikilia desturi zao za za-
mani. Hawamwabudu Mwenyezi Mungu wala
kuzishika hukumu na maagizo, sheria na amri
ambazo Mwenyezi Mungu aliwapa uzao wa
Yakobo, ambaye alimwita Israeli.
35 Mwenyezi Mungu alipofanya agano na Wais-
raeli, aliwaamuru: “Msiiabudu miungu mingine
yoyote wala kuisujudia, wala kuitumikia wala
kuitolea dhabihu.
36 Bali imewapasa kumwabudu Mwenyezi
Mungu aliyewapandisha kutoka Misri kwa
uwezo wake mkuu na kwa mkono wake
ulionyooshwa. Kwake yeye mtasujudu, na kwake
yeye mtatoa dhabihu.
37 Imewapasa daima kuwa waangalifu ku-
tunza hukumu na maagizo, sheria na amri ali-
zowaandikia. Msiabudu miungu mingine.
38 Msisahau agano nililofanya nanyi, wala msi-
abudu miungu mingine.

39 Bali, mtamwabudu Mwenyezi Mungu, Mungu wenu, kwani yeye ndiye atakayewakomboa kutoka mikononi mwa adui zenu wote.”
40 Hata hivyo hawakusikiliza, lakini waliendelea na desturi zao za awali.
41 Hata wakati watu hawa walipokuwa wanamwabudu Mwenyezi Mungu, walikuwa bado wakitumikia sanamu zao. Hadi leo watoto wao na wajukuu wao wanaendelea kufanya kama baba zao walivyofanya.

# 18

### *Hezekia mfalme wa Yuda*
### *(2 Nyakati 29:1–31:21)*

1 Katika mwaka wa tatu wa utawala wa Hoshea mwana wa Ela mfalme wa Israeli, Hezekia mwana wa Ahazi mfalme wa Yuda alianza kutawala.
2 Alikuwa na umri wa miaka ishirini na tano alipoanza kutawala, naye akatawala huko Yerusalemu kwa miaka ishirini na tisa. Mama yake aliitwa Abiya binti Zekaria.
3 Akafanya yaliyo mema machoni pa Mwenyezi Mungu, kama Daudi baba yake alivyofanya.
4 Akapaondoa mahali pa juu pa kuabudia, akazivunja sanamu, akakatakata nguzo za Ashera. Akavunja vipande vipande ile nyoka ya shaba Musa aliyotengeneza, kwa kuwa hadi siku hizo Waisraeli walikuwa wanaifukizia uvumba. (Ilikuwa ikiitwa Nehushtani*).
5 Hezekia aliweka tumaini lake kwa Mwenyezi Mungu, Mungu wa Israeli. Hapakuwa na mfalme

* **18:4** maana yake *Kipande cha shaba*

mwingine wa kufanana naye miongoni mwa
wafalme wa Yuda, kabla yake au baada yake.
6 Alishikamana na Mwenyezi Mungu kwa bidii
wala hakuacha kumfuata; alishika amri ambazo
Mwenyezi Mungu alikuwa amempa Musa.
7 Naye Mwenyezi Mungu alikuwa pamoja naye,
akafanikiwa katika kila alichokifanya. Aliasi
dhidi ya mfalme wa Ashuru, wala hakumtu-
mikia.
8 Kuanzia mnara wa ulinzi hadi kwenye mji
wenye ngome, aliwashinda Wafilisti, hadi kufikia
Gaza na himaya yake yote.
9 Mwaka wa nne wa Mfalme Hezekia, ambao
ulikuwa mwaka wa saba wa Hoshea mwana
wa Ela kutawala Israeli, Shalmanesa mfalme wa
Ashuru alienda kushambulia Samaria na kuuzin-
gira.
10 Baada ya miaka mitatu Waashuru wakaut-
waa. Kwa hiyo Samaria ulitekwa katika mwaka
wa sita wa utawala wa Mfalme Hezekia, ambao
ulikuwa mwaka wa tisa wa utawala wa Hoshea
mfalme wa Israeli.
11 Mfalme wa Ashuru akawahamishia Wais-
raeli huko Ashuru na akawaweka Hala, na
Gozani karibu na Mto Habori, na katika miji ya
Wamedi.
12 Hili lilitokea kwa sababu hawakumtii
Mwenyezi Mungu, Mungu wao, lakini walikuwa
wamevunja agano lake, yale yote ambayo Musa
mtumishi wa Mwenyezi Mungu aliwaamuru.
Hawakuzisikiliza amri wala kuzitimiza.
13 Katika mwaka wa kumi na nne wa utawala
wa Mfalme Hezekia, Senakeribu mfalme wa
Ashuru akaishambulia miji yote ya Yuda yenye
ngome na kuiteka.

14 Basi Hezekia mfalme wa Yuda akamtu-
mia ujumbe mfalme wa Ashuru huko Lakishi
akisema: “Nimefanya makosa. Ondoka katika
nchi yangu, nami nitakulipa chochote unachok-
itaka kwangu.” Mfalme wa Ashuru akamtoza
Hezekia mfalme wa Yuda talanta mia tatu† za
fedha, na talanta thelathini‡ za dhahabu.
15 Basi Hezekia akampa fedha yote
iliyopatikana ndani ya Hekalu la Mwenyezi
Mungu na katika hazina ya jumba la mfalme.

16 Wakati huu Hezekia mfalme wa Yuda aka-
bandua dhahabu yote iliyokuwa imefunika mi-
lango na miimo ya Hekalu la Mwenyezi Mungu,
akampa mfalme wa Ashuru.

### *Senakeribu anaitishia Yerusalemu*
### *(2 Nyakati 32:1-19; Isaya 36:1-22)*

17 Mfalme wa Ashuru akamtuma jemadari
wake mkuu, na afisa wake mkuu, na jemadari wa
jeshi, pamoja na jeshi kubwa kutoka Lakishi hadi
kwa Mfalme Hezekia huko Yerusalemu. Wakaja
Yerusalemu na kusimama kwenye mfereji wa
Bwawa la Juu, lililojengwa katika barabara ien-
dayo kwenye Uwanja wa Dobi.
18 Wakaagiza mfalme aitwe. Eliakimu mwana
wa Hilkia aliyekuwa msimamizi wa jumba
la mfalme, Shebna aliyekuwa katibu, na Yoa
mwana wa Asafu mwandishi wakawaendea.
19 Yule jemadari wa jeshi akawaambia,
“Mwambieni Hezekia:

† **18:14** Talanta 300 ni sawa na tani 10. ‡ **18:14** Talanta 30 ni sawa na tani moja.

" 'Hili ndilo asemalo mfalme mkuu, mfalme
wa Ashuru: Ni wapi unapoweka hili tumaini
lako?
20 Unasema mnayo mikakati na nguvu za
kijeshi, lakini unasema maneno matupu tu. Je,
wewe unamtegemea nani, hata ukaniasi mimi?
21 Tazama sasa, unaitegemea Misri, fimbo ile
ya mwanzi uliopasuka, ambayo huuchoma na
kuujeruhi mkono wa mtu akiiegemea! Hivyo
ndivyo alivyo Farao mfalme wa Misri, kwa wote
wanaomtegemea.
22 Nawe ukiniambia, "Tunamtumainia
Mwenyezi Mungu, Mungu wetu": je, siyo yeye
ambaye Hezekia aliondoa mahali pake pa juu
pa kuabudia na madhabahu zake, akiwaambia
Yuda na Yerusalemu, "Ni lazima mwabudu mbele
ya madhabahu haya katika Yerusalemu"?
23 " 'Njooni sasa, fanyeni mapatano na bwana
wangu, mfalme wa Ashuru: Nitakupa farasi
elfu mbili, kama unaweza kuwapandisha
waendesha farasi juu yao!
24 Utawezaje kumzuia hata afisa mmoja aliye
mdogo kati ya maafisa wa bwana wangu, ijapo
unategemea Misri kwa magari ya vita na wa-
panda farasi?
25 Zaidi ya hayo, je, nimekuja kushambulia
na kuangamiza mahali hapa pasipo neno ku-
toka kwa Mwenyezi Mungu? Mwenyezi Mungu
mwenyewe ndiye aliniambia niishambulie nchi
hii na kuiangamiza.' "

26 Ndipo Eliakimu mwana wa Hilkia, Shebna
na Yoa wakamwambia yule jemadari wa jeshi,
"Tafadhali zungumza na watumishi wako kwa

lugha ya Kiaramu, kwa kuwa tunaifahamu. Usiseme nasi kwa Kiebrania, watu walio juu ya ukuta wakiwa wanasikia.”

27 Lakini yule jemadari wa jeshi akajibu, “Je, bwana wangu amenituma kutoa ujumbe huu kwa bwana wenu na kwenu tu? Je, hakunituma pia kwa watu walioketi ukutani, ambao, kama ninyi, itawabidi kula mavi yao na kunywa mkojo wao wenyewe?”

28 Kisha yule jemadari wa jeshi akasimama na kuita kwa lugha ya Kiebrania, akasema: “Sikieni neno la mfalme mkuu, mfalme wa Ashuru!

29 Hili ndilo asemalo mfalme: Msikubali Hezekia awadanganye. Hawezi kuwaokoa mkononi mwangu.

30 Msikubali Hezekia awashawishi kumtumaini Mwenyezi Mungu kwa kuwaambia, ‘Hakika Mwenyezi Mungu atatuokoa. Mji huu hautaangukia mikononi mwa mfalme wa Ashuru.’

31 “Msimsikilize Hezekia. Hili ndilo mfalme wa Ashuru asemalo: Fanyeni amani nami na mje kwangu. Kisha kila mmoja wenu atakula kutoka kwa mzabibu wake na mtini wake mwenyewe, na kunywa maji kutoka kisima chake mwenyewe,

32 hadi nije nikawapeleke katika nchi iliyo kama nchi yenu wenyewe, nchi ya nafaka na divai mpya, nchi ya mkate na mashamba ya mizabibu, nchi ya mizeituni na asali. Chagueni uzima, sio mauti!

“Msimsikilize Hezekia, kwa kuwa anawapotosha asemapo, ‘Mwenyezi Mungu atatuokoa.’

33 Je, yuko mungu wa taifa lolote aliyewahi
kuokoa nchi yake kutoka mkononi mwa mfalme
wa Ashuru?
34 Iko wapi miungu ya Hamathi na ya Arpadi?
Iko wapi miungu ya Sefarvaimu, Hena na Iva? Je,
imeokoa Samaria kutoka mkononi mwangu?
35 Ni yupi miongoni mwa miungu yote ya
nchi hizi ameweza kuokoa nchi yake mkononi
mwangu? Inawezekanaje basi Mwenyezi Mungu
aiokoe Yerusalemu mkononi mwangu?"
36 Lakini wale watu wakakaa kimya, wala
hawakujibu lolote, kwa kuwa mfalme alikuwa
amewaamuru, "Msimjibu lolote."
37 Kisha Eliakimu mwana wa Hilkia msimamizi
wa jumba la kifalme, Shebna katibu, na Yoa
mwana wa Asafu, mwandishi wakamwendea
Hezekia, nguo zao zikiwa zimeraruliwa, na
kumwambia vile jemadari wa jeshi alivyosema.

# 19

### *Hezekia autafuta msaada wa Mwenyezi Mungu (Isaya 37:1-13)*

1 Mfalme Hezekia aliposikia haya, akararua
nguo zake na kuvaa gunia, naye akaenda katika
Hekalu la Mwenyezi Mungu.
2 Akawatuma Eliakimu msimamizi wa nyumba
ya mfalme, Shebna mwandishi, na viongozi wa
makuhani, wote wakiwa wamevaa magunia,
waende kwa nabii Isaya mwana wa Amozi.
3 Wakamwambia, "Hili ndilo asemalo Hezekia:
Siku hii ni siku ya dhiki, ya kukaripiwa na ya
aibu, kama wakati watoto wanapofikia karibu
kuzaliwa na kumbe hakuna nguvu ya kuwazaa.

4 Yamkini Mwenyezi Mungu, Mungu wako,
atayasikia maneno ya jemadari wa jeshi, am-
baye bwana wake, mfalme wa Ashuru, amem-
tuma kumdhihaki Mungu aliye hai, tena kwamba
atamkemea kwa maneno ambayo Mwenyezi
Mungu, Mungu wako, ameyasikia. Kwa hiyo
omba kwa ajili ya mabaki ambao bado wako."

5 Maafisa wa Mfalme Hezekia walipofika kwa
Isaya,
6 Isaya akawaambia, "Mwambieni bwana
wenu, 'Hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu:
Usiogope kwa hayo uliyoyasikia, yale maneno
ambayo watumishi wa mfalme wa Ashuru
wamenitukana nayo.
7 Sikiliza! Nitatia roho fulani ndani yake, naye
atakaposikia ujumbe fulani, atarudi nchi yake
mwenyewe; nami huko nitafanya auawe kwa
upanga.' "

8 Jemadari wa jeshi aliposikia kwamba
mfalme wa Ashuru ameondoka Lakishi, alirudi,
akamkuta mfalme akipigana na Libna.

9 Basi Senakeribu akapata taarifa kwamba
Tirhaka Mkushi, mfalme wa Misri, alikuwa
anaenda kupigana naye. Basi akatuma tena
wajumbe kwa Hezekia na neno hili:
10 "Mwambieni Hezekia mfalme wa Yuda:
Usikubali huyo Mungu unayemtumainia akudan-
ganye wakati anaposema, 'Yerusalemu haitatiwa
mkononi mwa mfalme wa Ashuru.'
11 Hakika umesikia yale ambayo wafalme
wa Ashuru wametenda kwa nchi zote, waki-
waangamiza kabisa. Je, wewe utaokolewa?

12 Je, miungu ya mataifa ambayo
yaliangamizwa na baba zangu iliweza
kuwaokoa, hiyo miungu ya Gozani, Harani,
Resefu, na ya watu wa Edeni waliokuwa Telasari?
13 Yuko wapi mfalme wa Hamathi, mfalme wa
Arpadi, mfalme wa mji wa Sefarvaimu, au wa
Hena au wa Iva?"

### *Maombi ya Hezekia*
### *(Isaya 37:14-20)*

14 Hezekia akapokea barua kutoka kwa wale
wajumbe, naye akaisoma. Kisha akapanda
katika Hekalu la Mwenyezi Mungu, akaikunjua
mbele za Mwenyezi Mungu.
15 Naye Hezekia akamwomba Mwenyezi
Mungu akisema: "Ee Mwenyezi Mungu, Mungu
wa Israeli, unayeketi kwenye kiti cha enzi kati
ya makerubi, wewe peke yako ndiwe Mungu juu
ya falme zote za dunia. Wewe umeumba mbingu
na nchi.
16 Tega sikio, Ee Mwenyezi Mungu, usikie;
fungua macho yako, Ee Mwenyezi Mungu, uone;
sikiliza maneno ambayo Senakeribu ametuma
kumtukana Mungu aliye hai.
17 "Ni kweli, Ee Mwenyezi Mungu, kwamba
wafalme wa Ashuru wameyaangamiza mataifa
haya na nchi zao.
18 Wameitupa miungu yao kwenye moto na
kuiangamiza, kwa kuwa haikuwa miungu, bali
miti na mawe tu iliyotengenezwa kwa mikono ya
wanadamu.
19 Sasa basi, Ee Mwenyezi Mungu, Mungu wetu,
tuokoe kutoka mkononi mwake, ili falme zote

duniani zipate kujua kwamba wewe peke yako, Ee Mwenyezi Mungu, ndiwe Mungu pekee."

### *Kuanguka kwa Senakeribu (Isaya 37:21-38)*

20 Kisha Isaya mwana wa Amozi akapeleka
ujumbe kwa Hezekia, akasema: "Hili ndilo ase-
malo Mwenyezi Mungu, Mungu wa Israeli: Nime-
sikia maombi yako kuhusu Senakeribu mfalme
wa Ashuru.
21 Hili ndilo neno ambalo Mwenyezi Mungu
amelisema dhidi yake:

" 'Bikira Binti Sayuni anakudharau na kukudhihaki.
Binti Yerusalemu anatikisa kichwa chake unapokimbia.
22 Ni nani uliyemtukana na kumkufuru?
Ni nani uliyepaza sauti yako dhidi yake,
na kumwinulia macho yako kwa kiburi?
Ni dhidi ya yule Aliye Mtakatifu wa Israeli!
23 Kupitia kwa wajumbe wako
umelundika matukano juu ya Bwana.
Nawe umesema,
"Kwa magari yangu mengi ya vita,
nimepanda juu ya vilele vya milima,
vilele vya juu sana katika Lebanoni.
Nami nimeiangusha mierezi yake mirefu,
misunobari yake iliyo bora sana.
Nimefikia sehemu zake zilizo mbali sana,
misitu yake iliyo mizuri sana.
24 Nimechimba visima katika nchi za kigeni
na kunywa maji yake.
Kwa nyayo za miguu yangu
nimekausha vijito vyote vya Misri."

25 “ ‘Je, hujasikia?
Zamani sana niliamuru hili.
Siku za kale nilipanga hili;
sasa nimelifanya litokee,
kwamba umegeuza miji yenye ngome
kuwa malundo ya mawe.
26 Watu wa miji hiyo wameishiwa nguvu,
wanavunjika mioyo na kuaibishwa.
Wao ni kama mimea katika shamba,
kama machipukizi mororo ya kijani,
kama majani yachipuayo juu ya paa la nyumba,
ambayo hukauka kabla ya kukua.

27 “ ‘Lakini ninajua mahali ukaapo,
kutoka kwako na kuingia kwako,
na jinsi unavyoghadhibika dhidi yangu.
28 Kwa sababu unaghadhibika dhidi yangu,
na ufidhuli wako umefika masikioni mwangu,
nitaweka ndoana yangu puani mwako
na hatamu yangu kinywani mwako,
nami nitakufanya urudi kwa njia ile uliyoijia.’

29 “Hii ndiyo itakuwa ishara kwako, ee Hezekia:
“Mwaka huu utakula kile kinachoota chenyewe,
na mwaka wa pili utakula kutoka machipukizi yake.
Lakini katika mwaka wa tatu, panda na uvune,
panda mashamba ya mizabibu na ule matunda yake.
30 Mara nyingine tena mabaki ya nyumba ya Yuda

wataeneza mizizi chini na kuzaa matunda juu.
31 Kwa kuwa kutoka Yerusalemu watakuja mabaki,
na kutoka Mlima Sayuni kundi la walionusurika.
Wivu wa Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni utatimiza jambo hili.

32 “Kwa hiyo hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu kuhusu mfalme wa Ashuru:

“Hataingia katika mji huu
wala hatapiga mshale hapa.
Hatakuja mbele yake akiwa na ngao,
wala kupanga majeshi kuuzingira.
33 Kwa njia ile aliyoijia, ndiyo atakayorudi;
hataingia katika mji huu,
asema Mwenyezi Mungu.
34 Nitaulinda mji huu na kuuokoa,
kwa ajili yangu mwenyewe,
na kwa ajili ya Daudi mtumishi wangu.”

35 Usiku ule, malaika wa Mwenyezi Mungu
akaenda, akawaua wanajeshi elfu mia moja na themanini na tano katika kambi ya Waashuru. Wenzao walipoamka asubuhi yake, walikuta maiti kila mahali!
36 Basi Senakeribu mfalme wa Ashuru
akavunja kambi na kuondoka. Akarudi Ninawi na kukaa huko.
37 Siku moja, alipokuwa akiabudu katika
hekalu la mungu wake Nisroki, wanawe Adrameleki na Shareza wakamuua kwa upanga,

nao wakakimbilia nchi ya Ararati. Naye Esar-
Hadoni mwanawe akawa mfalme baada yake.

# 20

### *Ugonjwa wa Hezekia*
### *(2 Nyakati 32:24-26; Isaya 38:1-8, 21-22)*

1 Katika siku hizo, Hezekia akaugua, naye
akawa karibu kufa. Nabii Isaya mwana wa
Amozi akaenda kwake na kumwambia, "Hili
ndilo asemalo Mwenyezi Mungu: Tengeneza
mambo ya nyumba yako, kwa sababu utakufa,
hutapona."

2 Hezekia akaelekeza uso wake ukutani, akam-
womba Mwenyezi Mungu:
3 "Ee Mwenyezi Mungu, kumbuka jinsi nilivy-
oenenda mbele zako kwa uaminifu na kuji-
toa kwa moyo wangu wote, na kufanya yaliyo
mema machoni pako." Naye Hezekia akalia kwa
uchungu.

4 Kabla Isaya hajaondoka katika ua wa kati,
neno la Mwenyezi Mungu likamjia, akaambiwa:
5 "Rudi ukamwambie Hezekia, kiongozi wa
watu wangu, 'Hili ndilo asemalo Mwenyezi
Mungu, Mungu wa baba yako Daudi:
Nimeyasikia maombi yako na nimeona machozi
yako; nitakuponya. Siku ya tatu kuanzia sasa
utapanda kwenda katika Hekalu la Mwenyezi
Mungu.
6 Nitakuongezea miaka kumi na tano katika
maisha yako. Nami nitakuokoa wewe pamoja
na mji huu kutoka mkononi mwa mfalme wa

Ashuru. Nitaulinda mji huu kwa ajili yangu, na kwa ajili ya mtumishi wangu Daudi!' "

7 Kisha Isaya akasema, "Tengenezeni dawa ya kubandika ya tini." Wakafanya hivyo na kuiweka kwenye jipu, naye akapona.

8 Hezekia alimuuliza Isaya, "Kutakuwa na ishara gani kwamba Mwenyezi Mungu ataniponya mimi, na kwamba nitapanda kwenda katika Hekalu la Mwenyezi Mungu siku ya tatu tangu leo?"

9 Isaya akajibu, "Hii ndiyo ishara ya Mwenyezi Mungu kwako kwamba Mwenyezi Mungu atafanya kile alichoahidi: Je, kivuli kiende hatua kumi mbele, au kivuli kirudi nyuma hatua kumi?"

10 Hezekia akasema, "Ni jambo rahisi kwa kivuli kutangulia mbele hatua kumi, kuliko kukifanya kirudi nyuma hatua kumi."

11 Ndipo nabii Isaya akamwita Mwenyezi Mungu, naye Mwenyezi Mungu akakifanya kivuli kurudi nyuma hatua kumi ambazo kilikuwa kimeshuka kwenye ngazi ya Ahazi.

### *Wajumbe kutoka Babeli (Isaya 39:1-8)*

12 Wakati huo Merodaki-Baladani, mwana wa Baladani mfalme wa Babeli, akamtumia Hezekia barua na zawadi, kwa sababu alikuwa amesikia habari za kuugua kwa Hezekia.

13 Hezekia akawapokea wale wajumbe na kuwaonesha vitu vyote vilivyokuwa katika ghala zake: yaani fedha, dhahabu, vikolezo na mafuta safi, ghala la silaha na kila kitu kilichokuwa

katika hazina yake. Hapakuwa na kitu katika
jumba lake la kifalme au katika ufalme wake
wote ambacho Hezekia hakuwaonesha.
14 Ndipo nabii Isaya akaenda kwa Mfalme
Hezekia na kumuuliza, “Watu hao walisema nini,
na wametoka wapi?”

Hezekia akamjibu, “Wametoka nchi ya mbali.
Walikuja kutoka Babeli.”

15 Nabii akauliza, “Waliona nini katika jumba
lako la kifalme?”
Hezekia akajibu, “Waliona kila kitu katika
jumba langu. Hakuna kitu katika hazina yangu
ambacho sikuwaonesha.”
16 Ndipo Isaya akamwambia Hezekia, “Sikia
neno la Mwenyezi Mungu:
17 Hakika wakati unakuja ambapo vitu vyote
katika jumba lako, na vyote ambavyo baba zako
waliweka akiba hadi siku hii, vitachukuliwa
kwenda Babeli. Hakuna chochote kitakachosalia,
asema Mwenyezi Mungu.
18 Nao baadhi ya wazao wako, mwili wako na
damu yako mwenyewe watakaozaliwa kwako,
watachukuliwa mateka, nao watakuwa ma-
towashi katika jumba la mfalme wa Babeli.”
19 Hezekia akamjibu Isaya, “Neno la Mwenyezi
Mungu ulilosema ni jema.” Kwa kuwa alifikiri, “Si
patakuwa na amani na usalama wakati wa uhai
wangu?”
20 Kuhusu matukio mengine ya utawala wa
Hezekia, mafanikio yake yote, na jinsi alivyoten-
geneza bwawa na mfereji ulioleta maji katika
mji, je, hayakuandikwa katika kitabu cha kum-
bukumbu za wafalme wa Yuda?

21 Hezekia akalala na baba zake. Naye Manase
mwanawe akawa mfalme baada yake.

# 21

### *Manase mfalme wa Yuda*
### *(2 Nyakati 33:1-20)*

1 Manase alikuwa na umri wa miaka kumi na
mbili alipoanza kutawala, naye akatawala huko
Yerusalemu miaka hamsini na tano. Mama yake
aliitwa Hefsiba.
2 Akafanya maovu machoni pa Mwenyezi
Mungu, akafuata desturi za machukizo za
mataifa ambayo Mwenyezi Mungu aliyafukuza
mbele ya Waisraeli.
3 Akajenga upya mahali pa juu pa kuabudia
ambapo Hezekia baba yake alikuwa amepabo-
moa. Pia akasimamisha madhabahu za Baali
na kutengeneza nguzo ya Ashera, kama Ahabu
mfalme wa Israeli alivyofanya. Akalisujudia
jeshi lote la angani na kuliabudu.
4 Akajenga madhabahu katika Hekalu
la Mwenyezi Mungu, ambamo Mwenyezi
Mungu alikuwa amesema, “Katika Yerusalemu
nitaliweka Jina langu.”
5 Katika nyua zote mbili za Hekalu la Mwenyezi
Mungu, akajenga madhabahu kwa ajili ya jeshi
lote la angani.
6 Akamtoa kafara mwanawe katika moto,
akafanya uchawi na uaguzi, na akataka shauri
kwa wapiga ramli na kwa mizimu. Akafanya
maovu mengi sana machoni mwa Mwenyezi
Mungu na kumghadhibisha.

7 Akachukua nguzo ya Ashera aliyoichonga
na kuiweka katika Hekalu, ambalo Mwenyezi
Mungu alikuwa amemwambia Daudi na
mwanawe Sulemani, "Katika Hekalu hili na
katika Yerusalemu, mji niliouchagua kutoka
makabila yote ya Israeli, nitaliweka Jina langu
milele.
8 Sitaifanya tena miguu ya Waisraeli itange-
tange kutoka nchi niliyowapa baba zao, ikiwa
watakuwa waangalifu kufanya kila kitu nili-
chowaamuru, na kuishika Torati yote ambayo
walipewa na Musa mtumishi wangu."
9 Lakini hawa watu hawakusikiliza. Manase
akawapotosha, kiasi kwamba walifanya maovu
mengi kuliko mataifa ambayo Mwenyezi Mungu
aliangamiza mbele ya Waisraeli.

10 Mwenyezi Mungu akasema kupitia watu-
mishi wake manabii:
11 "Manase mfalme wa Yuda ametenda dhambi
hizi za kuchukiza. Amefanya maovu mengi ku-
liko Waamori waliokuwa kabla yake, na ameion-
goza Yuda katika dhambi kwa sanamu zake.
12 Kwa hiyo hili ndilo asemalo Mwenyezi
Mungu, Mungu wa Israeli: Nitaleta maafa
makubwa juu ya Yerusalemu na Yuda, kiasi
kwamba masikio ya kila mmoja atakayesikia
habari zake yatawasha.
13 Nitanyoosha juu ya Yerusalemu kamba ya
kupimia iliyotumika dhidi ya Samaria, na timazi
iliyotumika dhidi ya nyumba ya Ahabu. Ni-
taifutilia mbali Yerusalemu kama mtu afutavyo
sahani, nikiifuta na kuifunikiza.
14 Nitawakataa mabaki wa urithi wangu

na kuwatia mikononi mwa adui zao. Watapokonywa mali yao na kutekwa nyara na adui zao wote,
15 kwa sababu wametenda uovu machoni pangu na kunighadhibisha tangu siku baba zao walipotoka Misri hadi leo."

16 Zaidi ya hayo, Manase pia alimwaga damu nyingi isiyo na hatia, hivi kwamba aliijaza Yerusalemu kutoka mwanzo hadi mwisho, mbali na dhambi ambayo alikuwa amesababisha Yuda kufanya, na hivyo wakatenda maovu machoni pa Mwenyezi Mungu.

17 Kuhusu matukio mengine ya utawala wa Manase, na yote aliyoyafanya, pamoja na dhambi alizotenda, je, hayakuandikwa katika kitabu cha kumbukumbu za wafalme wa Yuda?
18 Manase akalala na baba zake, akazikwa katika bustani ya jumba lake la kifalme, katika bustani ya Uza. Naye Amoni mwanawe akawa mfalme baada yake.

### *Amoni mfalme wa Yuda (2 Nyakati 33:21-25)*

19 Amoni alikuwa na umri wa miaka ishirini na mbili alipoanza kutawala, naye akatawala huko Yerusalemu kwa miaka miwili. Mamaye aliitwa Meshulemethi binti Haruzi, kutoka Yotba.
20 Akatenda maovu machoni mwa Mwenyezi Mungu, kama baba yake Manase alivyofanya.
21 Akaenenda katika njia zote za baba yake, akaabudu sanamu ambazo baba yake aliziabudu na kuzisujudia.

22 Akamwacha Mwenyezi Mungu, Mungu wa
baba zake, wala hakuenenda katika njia za
Mwenyezi Mungu.
23 Watumishi wa Amoni wakampangia njama,
nao wakamuua ndani ya jumba lake la kifalme.
24 Kisha watu wa nchi wakawaua wale wote
waliokuwa wamepanga njama dhidi ya Mfalme
Amoni. Wakamfanya Yosia mwanawe kuwa
mfalme mahali pake.
25 Kuhusu matukio mengine ya utawala wa
Amoni na yale aliyoyafanya, je, hayakuandikwa
katika kitabu cha kumbukumbu za wafalme wa
Yuda?
26 Akazikwa kwenye kaburi lake katika bustani
ya Uza. Naye Yosia mwanawe akawa mfalme
baada yake.

# 22

*Yosia mfalme wa Yuda*
*(2 Nyakati 34; 35:20-27)*

1 Yosia alikuwa na umri wa miaka nane
alipoanza kutawala, naye akatawala huko
Yerusalemu miaka thelathini na moja. Mama
yake aliitwa Yedida binti Adaya, kutoka Boskathi.
2 Akafanya yaliyo mema machoni pa Mwenyezi
Mungu na kuenenda katika njia zote za Daudi
baba yake. Hakugeuka upande wa kuume wala
wa kushoto.
3 Katika mwaka wa kumi na nane wa
utawala wake, Mfalme Yosia akamtuma
mwandishi Shafani mwana wa Azalia, mwana
wa Meshulamu, kwenda katika Hekalu la
Mwenyezi Mungu. Akasema:

4 “Panda uende kwa Hilkia, kuhani mkuu, umwambie ahesabu zile fedha ambazo zimeletwa katika Hekalu la Mwenyezi Mungu, ambazo mabawabu wamekusanya kutoka kwa watu.

5 Waambie waikabidhi kwa watu walioteuliwa kusimamia kazi ya Hekalu. Waamuru watu hawa wawalipe wafanyakazi ambao wanakarabati Hekalu la Mwenyezi Mungu:

6 wale maseremala, wajenzi na waashi. Waambie pia wanunue mbao na mawe yaliyochongwa ili kukarabati Hekalu.

7 Lakini hawahitajiki kutoa maelezo ya fedha walizokabidhiwa, kwa sababu wanafanya kazi kwa uaminifu.”

8 Hilkia kuhani mkuu akamwambia Shafani mwandishi, “Nimekipata Kitabu cha Torati ndani ya Hekalu la Mwenyezi Mungu.” Akampa Shafani, ambaye alikisoma.

9 Kisha Shafani mwandishi akamwendea mfalme na kumpa taarifa akisema: “Maafisa wako wametoa ile fedha ambayo ilikuwa ndani ya Hekalu la Mwenyezi Mungu na imekabidhiwa mikononi mwa wasimamizi wa marekebisho ya Hekalu.”

10 Ndipo Shafani mwandishi akampasha mfalme habari, akisema: “Hilkia kuhani amenipa kitabu hiki.” Naye Shafani akakisoma kile kitabu mbele ya mfalme.

11 Mfalme aliposikia maneno ya kile Kitabu cha Torati, akararua mavazi yake.

12 Akatoa maagizo haya kwa Hilkia kuhani, Ahikamu mwana wa Shafani, Akbori mwana wa

Mikaya, Shafani mwandishi, na Asaya mtumishi wa mfalme:
13 "Nendeni mkamuulize Mwenyezi Mungu kwa ajili yangu, na kwa ajili ya watu na Yuda wote kuhusu yale yaliyoandikwa ndani ya kitabu hiki ambacho kimepatikana. Hasira ya Mwenyezi Mungu ni kubwa inayowaka dhidi yetu kwa sababu baba zetu hawakuyatii maneno ya kitabu hiki. Hawajatenda kulingana na yale yote yaliyoandikwa humo kutuhusu."

14 Hilkia kuhani, Ahikamu, Akbori, Shafani na Asaya wakaenda kuongea na nabii mke Hulda, aliyekuwa mke wa Shalumu mwana wa Tikwa, mwana wa Harhasi mtunzaji wa chumba cha mavazi. Hulda aliishi Yerusalemu katika Mtaa wa Pili.

15 Akawaambia, "Hivi ndivyo asemavyo Mwenyezi Mungu, Mungu wa Israeli: Mwambieni yule mtu aliyewatuma ninyi kwangu,
16 'Hivi ndivyo asemavyo Mwenyezi Mungu: Nitaleta maafa juu ya mahali hapa na watu wake, kulingana na kila kitu kilichoandikwa katika kitabu hicho mfalme wa Yuda alichosoma.
17 Kwa sababu wameniacha mimi na kufukiza uvumba kwa miungu mingine, na kunighadhibisha kwa sanamu zote zilizotengenezwa kwa mikono yao, hasira yangu itawaka dhidi ya mahali hapa, wala haitatulizwa.'
18 Mwambieni mfalme wa Yuda, ambaye amewatuma kumuuliza Mwenyezi Mungu, 'Hivi ndivyo asemavyo Mwenyezi Mungu, Mungu wa Israeli, kuhusu maneno uliyoyasikia:

19 Kwa kuwa moyo wako ulikuwa msikivu na
ulijinyenyekeza mbele za Mwenyezi Mungu uli-
posikia kile nilichosema dhidi ya mahali hapa na
watu wake, kwamba wangelaaniwa na kuachwa
ukiwa, basi kwa sababu uliyararua mavazi
yako na kulia mbele zangu, nimekusikia, asema
Mwenyezi Mungu.
20 Kwa hiyo nitakukusanya kwa baba zako,
nawe utazikwa kwa amani. Macho yako hay-
ataona maafa yote nitakayoleta juu ya mahali
hapa.' "

Basi wakapeleka jibu lake kwa mfalme.

# 23

*Yosia analifanya upya agano*
*(2 Nyakati 34:3-7, 29-33)*

1 Kisha mfalme akawaita pamoja wazee wote
wa Yuda na Yerusalemu.
2 Akapanda kwenda hekaluni mwa Mwenyezi
Mungu pamoja na watu wa Yuda, watu wa
Yerusalemu, makuhani na manabii, watu wote
wakubwa kwa wadogo. Akasoma wakiwa
wanasikia maneno yote ya Kitabu cha Agano,
kilichokuwa kimepatikana katika Hekalu la
Mwenyezi Mungu.
3 Mfalme akasimama karibu na nguzo, na
kufanya upya agano mbele za Mwenyezi
Mungu: kwamba atamfuata Mwenyezi Mungu
na kuzishika amri zake, maagizo na sheria
zake kwa moyo wake wote na kwa roho yake
yote, na hivyo kuyathibitisha maneno ya agano
yaliyoandikwa katika kitabu hiki. Kisha watu

wote wakajifunga wenyewe kwa kiapo katika agano.

4 Mfalme akamwamuru Hilkia kuhani mkuu,
makuhani waliomfuata kwa cheo, na mabawabu
kuondoa kutoka Hekalu la Mwenyezi Mungu
vyombo vyote vilivyofanywa kwa ajili ya Baali na
Ashera na jeshi lote la mianga ya angani! Akavi-
choma nje ya Yerusalemu katika mashamba ya
Bonde la Kidroni, na kuyachukua hayo majivu
hadi Betheli.
5 Akawafukuza makuhani wa kipagani
waliokuwa wameteuliwa na wafalme wa Yuda
kufukiza uvumba katika mahali pa juu pa
kuabudia katika miji ya Yuda na ile iliyozunguka
Yerusalemu, yaani wale waliofukiza uvumba
kwa Baali, kwa jua na mwezi, kwa makundi ya
nyota, na jeshi lote la angani.
6 Akaiondoa nguzo ya Ashera kutoka Hekalu la
Mwenyezi Mungu, na kuipeleka kwenye Bonde
la Kidroni nje ya Yerusalemu, akaiteketeza huko.
Akaisaga hadi ikawa unga na kusambaza hilo
vumbi juu ya makaburi ya watu wasio na cheo.
7 Akabomoa pia nyumba za mahanithi wa
mahali pa ibada, zilizokuwa ndani ya Hekalu la
Mwenyezi Mungu, nyumba ambazo wanawake
walifumia pazia kwa ajili ya Ashera.

8 Yosia akawaleta makuhani wote wa
Mwenyezi Mungu kutoka miji yote ya Yuda,
na kunajisi mahali pa juu pa kuabudia, kuanzia
Geba hadi Beer-Sheba, mahali pote ambapo
hao makuhani wa miungu walifukiza uvumba.
Akabomoa mahali pa kuwekea vitu vya ibada
za miungu palipokuwa katika malango, kwenye

ingilio la Lango la Yoshua, mtawala wa mji,
lililoko upande wa kushoto wa lango la mji.
9 Ingawa makuhani wa mahali pa juu pa
kuabudia hawakuhudumu katika madhabahu ya
Mwenyezi Mungu katika Yerusalemu, walikula
mikate isiyotiwa chachu pamoja na ndugu zao.

10 Kisha mfalme akapanajisi Tofethi,
palipokuwa katika Bonde la Ben-Hinomu, ili
mtu yeyote asiweze kupatumia kumtoa kafara
mwanawe wa kiume au wa kike katika moto
kwa Moleki.
11 Akaondoa kutoka ingilio la Hekalu la
Mwenyezi Mungu wale farasi ambao wafalme
wa Yuda walikuwa wamewaweka wakfu kwa
ajili ya jua. Walikuwa kwenye ua karibu na
chumba cha afisa aliyeitwa Nathan-Meleki. Basi
Yosia akayachoma moto yale magari ya vita
yaliyokuwa yamewekwa wakfu kwa jua.

12 Alizivunja madhabahu ambazo wafalme wa
Yuda walikuwa wamezijenga kwenye paa la gho-
rofa ya Ahazi, pia madhabahu alizokuwa amez-
ijenga Manase katika nyua mbili za Hekalu la
Mwenyezi Mungu. Akaziondoa huko, akazivunja
vipande vipande, na kutupa hicho kifusi katika
Bonde la Kidroni.
13 Mfalme pia akanajisi mahali pa juu pa
kuabudia miungu, zilizokuwa mashariki mwa
Yerusalemu upande wa kusini wa Kilima cha
Uharibifu, ambapo Sulemani mfalme wa Israeli
alikuwa amejenga mahali pa kuabudia kwa ajili
ya Ashtorethi mungu wa kike wa Wasidoni,
aliyekuwa chukizo; na kwa ajili ya Kemoshi
mungu wa Wamoabu, aliyekuwa chukizo; na

kwa ajili ya Moleki mungu wa watu wa Amoni,
aliyekuwa chukizo.
14 Yosia akapasua yale mawe ya kuabudiwa na
kuzikatakata nguzo za Ashera. Kisha akafunika
hayo maeneo kwa mifupa ya wanadamu.
15 Hata madhabahu yaliyokuwa huko Betheli,
mahali pa juu pa kuabudia palipokuwa pame-
jengwa na Yeroboamu mwana wa Nebati, am-
baye aliwafanya Israeli watende dhambi, alibo-
moa hata hayo madhabahu na mahali pa juu pa
kuabudia. Alipateketeza kwa moto hapo mahali
pa juu pa kuabudia na kupasaga hadi pakawa
vumbi, na kuichoma hiyo nguzo ya Ashera pia.
16 Kisha Yosia akatazama huku na huko, naye
alipoona makaburi yaliyokuwa kwenye kilima,
akaamuru mifupa itolewe humo na akaichoma
juu ya madhabahu ya Betheli ili kupanajisi.
Hili lilitendeka kulingana na neno la Mwenyezi
Mungu lililosemwa na mtu wa Mungu ambaye
alitangulia kusema mambo haya.
17 Mfalme akauliza, “Lile kaburi lenye mnara
wa ukumbusho ninaloliona ni kwa ajili gani?”
Watu wa mji wakasema, “Hii ni alama ya
kaburi la mtu wa Mungu aliyekuja kutoka Yuda,
naye akanena dhidi ya madhabahu ya Betheli
mambo yale yale uliyoifanyia leo.”
18 Akasema, “Liacheni, msiliguse. Msimruhusu
mtu yeyote kuiondoa mifupa yake.” Basi waka-
iacha mifupa yake pamoja na ile ya yule nabii
aliyekuwa amekuja kutoka Samaria.
19 Kama alivyokuwa amefanya huko Betheli,
Yosia akabomoa nyumba za ibada katika ma-
hali pa juu pa kuabudia, ambazo wafalme wa

Israeli walikuwa wamejenga ndani ya miji ya Samaria, na ambazo zilikuwa zimemghadhibisha Mwenyezi Mungu.
20 Yosia akawachinja makuhani wote wa mahali pa juu pa kuabudia katika madhabahu zao wenyewe, na kuchoma mifupa ya wanadamu juu yake. Kisha akarudi Yerusalemu.

### *Yosia aadhimisha Pasaka*

21 Mfalme akatoa agizo hili kwa watu wote: "Adhimisheni Pasaka kwa Mwenyezi Mungu, Mungu wenu, kama ilivyoandikwa katika Kitabu hiki cha Agano."
22 Hapakuwahi kuwa na adhimisho lingine la Pasaka kama hilo tangu nyakati za waamuzi walioamua Israeli, wala katika nyakati zote za wafalme wa Israeli na wafalme wa Yuda.
23 Lakini katika mwaka wa kumi na nane wa utawala wa Mfalme Yosia, Pasaka hii iliadhimishwa kwa Mwenyezi Mungu huko Yerusalemu.
24 Zaidi ya hayo, Yosia akawaondoa waaguzi, waabudu mizimu, miungu ya nyumbani, sanamu za kuabudiwa, na vitu vingine vyote vya machukizo vilivyoonekana huko Yuda na Yerusalemu. Aliyafanya haya ili kutimiza matakwa ya sheria iliyoandikwa katika kile kitabu ambacho Hilkia kuhani alikipata ndani ya Hekalu la Mwenyezi Mungu.
25 Hapakuwepo mfalme mwingine kabla na baada ya Yosia aliyempenda Mwenyezi Mungu kama yeye; kwa moyo wake wote, kwa roho yake yote, na kwa nguvu zake zote, kulingana na Torati yote ya Musa.

26 Hata hivyo, Mwenyezi Mungu hakuacha
ghadhabu yake iliyowaka dhidi ya Yuda kwa
sababu ya yale yote ambayo Manase alikuwa
amefanya kumghadhibisha.
27 Hivyo Mwenyezi Mungu akasema, “Nitam-
wondoa Yuda mbele zangu kama nilivyomwon-
doa Israeli, nami nitaukataa Yerusalemu, mji
niliouchagua, na Hekalu hili, ambalo nilisema,
‘Jina langu litakaa humo.’ ”
28 Kuhusu matukio mengine ya utawala wa
Yosia na yote aliyoyafanya, je, hayakuandikwa
katika kitabu cha kumbukumbu za wafalme wa
Yuda?
29 Yosia alipokuwa mfalme, Farao Neko mfalme
wa Misri akapanda hadi Mto Frati kumsaidia
mfalme wa Ashuru. Mfalme Yosia akatoka
kwenda kupigana naye, lakini Neko akamkabili
na kumuua huko Megido.
30 Watumishi wa Yosia wakauleta mwili
wake katika gari la vita kutoka Megido hadi
Yerusalemu, wakamzika kwenye kaburi lake
mwenyewe. Nao watu wa nchi wakamchukua
Yehoahazi mwana wa Yosia, wakampaka mafuta
na kumfanya mfalme mahali pa baba yake.

### *Yehoahazi mfalme wa Yuda (2 Nyakati 36:2-4)*

31 Yehoahazi alikuwa na umri wa miaka
ishirini na tatu alipoanza kutawala, naye
akatawala huko Yerusalemu kwa miezi mitatu.
Mama yake aliitwa Hamutali binti Yeremia
kutoka Libna.
32 Akafanya maovu machoni mwa Mwenyezi
Mungu, kama baba zake walivyofanya.

33 Farao Neko akamfunga kwa minyororo
huko Ribla katika nchi ya Hamathi ili asiweze
kutawala huko Yerusalemu, naye akatoza kodi ya
talanta mia moja* za fedha, na talanta moja† ya
dhahabu katika Yuda.

### *Yehoyakimu mfalme wa Yuda (2 Nyakati 36:5-8)*

34 Farao Neko akamfanya Eliakimu mwana
wa Yosia kuwa mfalme mahali pa baba yake
Yosia, na kulibadilisha jina la Eliakimu kuwa
Yehoyakimu. Lakini akamchukua Yehoahazi na
kumpeleka Misri, naye akafia huko.
35 Yehoyakimu akamlipa Farao Neko ile fedha
na dhahabu aliyodai. Ili kuweza kufanya hivyo,
Yehoyakimu akatoza nchi kodi na kulipiza fedha
na dhahabu kutoka kwa watu wa nchi kulingana
na makadirio ya mapato yao.
36 Yehoyakimu alikuwa na umri wa miaka
ishirini na tano alipoanza kutawala, naye
akatawala huko Yerusalemu miaka kumi na
moja. Mama yake aliitwa Zebida binti Pedaya
kutoka Ruma.
37 Naye akafanya maovu machoni mwa
Mwenyezi Mungu, kama baba zake walivyokuwa
wamefanya.

## 24

1 Wakati wa utawala wa Yehoyakimu,
Nebukadneza mfalme wa Babeli aliishambulia
nchi, naye Yehoyakimu akawa mtumwa wake

* **23:33** Talanta 100 ni sawa na tani 3.4. † **23:33** Talanta moja ni sawa na kilo 34.

kwa miaka mitatu. Lakini hatimaye akabadili
mawazo yake na kuasi dhidi ya Nebukadneza.
2 Mwenyezi Mungu akatuma wavamiaji wa
Wakaldayo, Waaramu, Wamoabu na Waamoni
ili kumshambulia. Aliwatuma kuiangamiza
Yuda sawasawa na neno la Mwenyezi Mungu
lililosemwa na watumishi wake manabii.
3 Hakika mambo haya yalitokea Yuda kulin-
gana na agizo la Mwenyezi Mungu, ili kuwaon-
doa kutoka machoni pake kwa sababu ya dhambi
za Manase na yote aliyoyafanya,
4 ikiwa ni pamoja na kumwaga damu isiyo na
hatia. Kwa kuwa aliijaza Yerusalemu kwa damu
isiyo na hatia, naye Mwenyezi Mungu hakuwa
radhi kusamehe.
5 Kuhusu matukio mengine ya utawala
wa Yehoyakimu na yote aliyoyafanya, je,
hayakuandikwa katika kitabu cha kumbukumbu
za wafalme wa Yuda?
6 Yehoyakimu akalala na baba zake. Naye
Yehoyakini mwanawe akawa mfalme baada
yake.
7 Mfalme wa Misri hakutoka tena katika nchi
yake, kwa sababu mfalme wa Babeli alikuwa
ameitwaa himaya yake yote, kuanzia Kijito cha
Misri hadi Mto Frati.

### *Yehoyakini mfalme wa Yuda (2 Nyakati 36:9-10)*

8 Yehoyakini alikuwa na umri wa miaka
kumi na nane alipoanza kutawala, naye
akatawala huko Yerusalemu miezi mitatu. Mama
yake aliitwa Nehushta binti Elnathani kutoka
Yerusalemu.

9 Akafanya maovu machoni pa Mwenyezi Mungu, kama vile baba yake alivyokuwa amefanya.

10 Wakati huo, maafisa wa Nebukadneza mfalme wa Babeli walikuja kushambulia Yerusalemu, nao wakauzingira kwa jeshi.
11 Nebukadneza mwenyewe akaupandia mji wakati maafisa wake walipokuwa wameuzingira.
12 Yehoyakini mfalme wa Yuda, mama yake, wahudumu wake, wakuu na maafisa wake wote wakajisalimisha kwa Nebukadneza.

Katika mwaka wa nane wa utawala wa mfalme wa Babeli, akamchukua Yehoyakini kuwa mfungwa.
13 Kama vile Mwenyezi Mungu alivyokuwa amesema, Nebukadneza akaondoa hazina yote kutoka Hekalu la Mwenyezi Mungu na kutoka jumba la mfalme, akavichukua vyombo vyote vya dhahabu ambavyo Sulemani mfalme wa Israeli alikuwa amevitengeneza kwa ajili ya Hekalu la Mwenyezi Mungu.
14 Akawachukua watu wa Yerusalemu wote kwenda uhamishoni: yaani maafisa wote na wapiganaji, watu wenye ustadi wa ufundi na wahunzi, jumla yao watu elfu kumi. Watu maskini sana tu ndio walibaki katika nchi.

15 Nebukadneza akamchukua mateka Yehoyakini hadi Babeli. Pia akawachukua utumwani kutoka Yerusalemu hadi Babeli mama yake mfalme, wake zake, maafisa wake, na viongozi wote wa nchi.

16 Mfalme wa Babeli pia akawahamishia Babeli
wapiganaji elfu saba wenye nguvu na tayari kwa
vita, na mafundi na wahunzi elfu moja.
17 Akamfanya Matania, ndugu wa baba yake
Yehoyakini, kuwa mfalme mahali pake, na
akalibadilisha jina lake kuwa Sedekia.

### *Sedekia mfalme wa Yuda*
### *(2 Nyakati 36:11-12; Yeremia 52:1-3)*

18 Sedekia alikuwa na umri wa miaka ishirini
na moja alipoanza kutawala, naye akatawala
huko Yerusalemu miaka kumi na moja. Mama
yake aliitwa Hamutali binti Yeremia, kutoka
Libna.
19 Alifanya maovu machoni pa Mwenyezi
Mungu, kama alivyofanya Yehoyakimu.
20 Haya yote yalitendeka Yerusalemu na Yuda
kwa sababu ya hasira ya Mwenyezi Mungu, naye
mwishoni akawaondoa mbele zake.

Basi, Sedekia akaasi dhidi ya mfalme wa Babeli.

# 25

### *Kuanguka kwa Yerusalemu*
### *(2 Nyakati 36:13-21; Yeremia 52:3-30)*

1 Hivyo katika mwaka wa tisa wa utawala
wa Sedekia, katika siku ya kumi ya mwezi wa
kumi, Nebukadneza mfalme wa Babeli, akiwa na
jeshi lake lote, alifanya vita dhidi ya Yerusalemu.
Akapiga kambi nje ya mji na kuuzingira pande
zote.
2 Mji ulizingirwa na jeshi hadi mwaka wa kumi
na moja wa utawala wa Mfalme Sedekia.

3 Ilipofika siku ya tisa ya mwezi wa nne, njaa ikazidi kuwa kali sana ndani ya mji, hadi hapakuwa na chakula kwa ajili ya watu.
4 Kisha ukuta wa mji ukavunjwa, na jeshi lote likakimbia. Wakaondoka mjini usiku kupitia lango lililokuwa kati ya kuta mbili karibu na bustani ya mfalme, ingawa Wakaldayo walikuwa wameuzunguka mji. Wakakimbia kuelekea Araba.
5 Lakini jeshi la Wakaldayo likamfuatia mfalme na kumpata katika nchi tambarare za Yeriko. Askari wake wote wakatengwa naye na kutawanyika,
6 naye akakamatwa. Akapelekwa kwa mfalme wa Babeli huko Ribla, ambapo hukumu yake ilitangazwa.
7 Wakawaua wana wa Sedekia mbele ya macho yake. Kisha wakayang'oa macho yake, wakamfunga kwa pingu za shaba na kumpeleka Babeli.

8 Siku ya saba ya mwezi wa tano, katika mwaka wa kumi na tisa wa utawala wa Nebukadneza mfalme wa Babeli, Nebuzaradani mkuu wa askari walinzi wa mfalme, afisa wa mfalme wa Babeli, alikuja Yerusalemu.
9 Alichoma moto Hekalu la Mwenyezi Mungu, jumba la kifalme, na nyumba zote za Yerusalemu. Aliteketeza kila jengo muhimu.
10 Jeshi lote la Wakaldayo, chini ya mkuu wa askari walinzi wa mfalme, walivunja kuta zilizoizunguka Yerusalemu.
11 Nebuzaradani mkuu wa askari walinzi akawapeleka uhamishoni watu waliokuwa wamebaki katika mji, pamoja na mabaki ya

watu wa kawaida, na wale waliojisalimisha kwa mfalme wa Babeli.
12 Lakini yule jemadari wa askari walinzi akawaacha baadhi ya wale watu maskini kabisa ili watunze mashamba ya mizabibu na mashamba mengine.

13 Wakaldayo walivunja vipande vipande zile nguzo za shaba, vile vishikilio vya shaba vilivyohamishika, na ile Bahari ya shaba, ambavyo vyote vilikuwa katika Hekalu la Mwenyezi Mungu. Hivyo wakaichukua hiyo shaba na kuipeleka Babeli.
14 Wakachukua pia vyungu, masepetu, mikasi ya kusawazishia tambi, sahani na vyombo vyote vya shaba vilivyotumika katika huduma ya Hekalu.
15 Mkuu wa askari walinzi wa mfalme akachukua vile vyetezo na yale mabakuli ya kunyunyizia, vitu vyote vile vilivyokuwa vimetengenezwa kwa dhahabu safi au fedha.

16 Shaba iliyotokana na zile nguzo mbili, ile Bahari na vile vishikilio vilivyohamishika, ambavyo Sulemani alikuwa ametengeneza kwa ajili ya Hekalu la Mwenyezi Mungu, ilikuwa na uzito mwingi usioweza kupimika.
17 Kila nguzo ilikuwa na urefu wa dhiraa kumi na nane*. Sehemu ya shaba juu ya nguzo moja ilikuwa na urefu wa dhiraa tatu† na ilikuwa imepambwa kwa wavu na makomamanga ya shaba kuizunguka kote. Ile nguzo nyingine

* **25:17** Dhiraa 18 ni sawa na mita 8.2. † **25:17** Dhiraa 3 ni sawa na mita 1.35.

pamoja na wavu wake ilifanana na hiyo ya
kwanza.
18 Yule mkuu wa askari walinzi akawachukua
kama wafungwa Seraya kuhani mkuu, kuhani
Sefania aliyefuata kwa cheo, na mabawabu
watatu.
19 Miongoni mwa wale watu waliokuwa wame-
salia katika mji, alimchukua kiongozi wa wapi-
ganaji, na washauri watano wa mfalme. Akam-
chukua pia mwandishi aliyesimamia uandik-
ishaji wa watu wa nchi, pamoja na watu wake
sitini waliopatikana ndani ya mji.
20 Nebuzaradani jemadari akawachukua hao
wote na kuwapeleka kwa mfalme wa Babeli huko
Ribla.
21 Huko Ribla, katika nchi ya Hamathi, mfalme
wa Babeli akaamuru wanyongwe.

Hivyo Yuda wakaenda utumwani mbali na
nchi yao.

22 Nebukadneza mfalme wa Babeli akam-
teua Gedalia mwana wa Ahikamu, mwana wa
Shafani, awe msimamizi wa watu aliowaacha
Yuda.
23 Maafisa wote wa jeshi na watu wao wali-
posikia kwamba mfalme wa Babeli amemteua
Gedalia kuwa mtawala, wakamjia Gedalia huko
Mispa. Hawa walikuwa Ishmaeli mwana wa
Nethania, Yohanani mwana wa Karea, Seraya
mwana wa Tanhumethi Mnetofathi, na Yezania
mwana wa Mmaaka, pamoja na watu wao.
24 Gedalia akaapa ili kuwatia moyo wao na
watu wao. Akasema, “Msiwaogope maafisa wa
Wakaldayo. Kaeni katika nchi na kumtumikia
mfalme wa Babeli, na itakuwa vyema kwenu.”

25 Hata hivyo, katika mwezi wa saba Ish-
maeli mwana wa Nethania mwana wa Elishama,
aliyekuwa wa uzao wa mfalme, akaja pamoja na
watu kumi, nao wakamuua Gedalia, na pia watu
wa Yuda, pamoja na Wakaldayo waliokuwa naye
huko Mispa.
26 Baada ya haya, watu wote kuanzia aliye
mdogo sana hadi aliye mkubwa kabisa, pamoja
na maafisa wa jeshi, wakakimbilia Misri kwa
kuwaogopa Wakaldayo.

### *Yehoyakini anaachiwa (Yeremia 52:31-34)*

27 Katika mwaka wa thelathini na saba tangu
Yehoyakini mfalme wa Yuda apelekwe uhamis-
honi, katika mwaka ule ambao Evil-Merodaki‡
alifanyika mfalme wa Babeli, alimwacha huru
Yehoyakini kutoka gerezani siku ya ishirini na
saba ya mwezi wa kumi na mbili.
28 Alizungumza naye kwa upole na kumpa kiti
cha heshima kuliko wafalme wengine aliokuwa
nao huko Babeli.
29 Hivyo Yehoyakini akayavua mavazi yake ya
gerezani, na siku zote za maisha yake zilizobaki
alikula mezani mwa mfalme.
30 Siku kwa siku mfalme alimpa Yehoyakini
posho siku zote za maisha yake.

‡ **25:27** au *Ameli-Mariduki*

# Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu

## The Holy Bible in Swahili: Open Neno: Maandiko Matakatifu 2024

copyright © 2018, 2024 Biblica, Inc.

Language: Kiswahili (Swahili)

Contributor: Biblica, Inc.

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

**Creative Commons License**

Kazi hii imewezeshwa kupitia idhini ya kundi la the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). Ili kuona nakala ya idhini hii, angalia kwenye anwani tovuti ya http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 au uandike barua kwa Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® ni alama ya biashara iliyosajilishwa na shirika la Biblica, Inc; unahitaji ruhusa ya kimaandiko kutoka kwa Biblica, Inc. ili kutumia alama ya biashara ya Biblica®. Kulingana na makubaliano ya leseni ya CC BY-SA, unaweza kutoa nakala na kusambaza kazi hii bila kuibadilisha kamwe, mradi tu udumishe alama ya biashara ya Biblica®. Ukibadilisha au kufasiri kazi hii, na hivyo ukanyambua kazi tofauti, sharti uondoe alama ya biashara ya Biblica®. Katika kazi uliyonyambua, sharti uarifu mabadiliko yako, na kutambua kazi yako hivi: "Kazi ya asili ya Biblica, Inc. inapatikana bila bei katika tovuti zawww.biblica.com na open.bible."

Ilani ya hakimiliki sharti iwe katika ukurasa wa kichwa au wa hakilimiliki kama ifuatavyo:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

Sharti pia uwasilishe kazi uliyonyambua kupitia kwa liseni hiyo hiyo ya CC BY-SA.

Ikiwa ungependa kujulisha Biblica, Inc. kuhusu tafsiri yako ya kazi hii, tafadhali wasiliana nasi katika tovuti https://open.bible/contact-us.

This work is made available under the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). To view a copy of this license, visit http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 or send a letter to Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® is a trademark registered by Biblica, Inc., and use of the Biblica® trademark requires the written permission of Biblica, Inc. Under the terms of the CC BY-SA license, you may copy and redistribute this unmodified work as long as you keep the Biblica® trademark intact. If you modify a copy or translate this work, thereby creating a derivative work, you must remove the Biblica® trademark. On the derivative work, you must indicate what changes you have made and attribute the work as follows: "The original work by Biblica, Inc. is available for free atwww.biblica.com and open.bible."

Notice of copyright must appear on the title or copyright page of the work as follows:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™

Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.

Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™

Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

You must also make your derivative work available under the same license (CC BY-SA).

If you would like to notify Biblica, Inc. regarding your translation of this work, please contact us at https://open.bible/contact-us.

This translation is made available to you under the terms of the Creative Commons Attribution Share-Alike license 4.0.

You have permission to share and redistribute this Bible translation in any format and to make reasonable revisions and adaptations of this translation, provided that:

You include the above copyright and source information.

If you make any changes to the text, you must indicate that you did so in a way that makes it clear that the original licensor is not necessarily endorsing your changes.

If you redistribute this text, you must distribute your contributions under the same license as the original.

Pictures included with Scriptures and other documents on this site are licensed just for use with those Scriptures and documents. For other uses, please contact the respective copyright owners.

Note that in addition to the rules above, revising and adapting God's Word involves a great responsibility to be true to God's Word. See Revelation 22:18-19.

2025-05-21

---

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 20 May 2025 from source files dated 21 May 2025

72687ba8-7233-577d-bf23-786df16f869d